

**Mzee** Abdul aapa kutomsamehe Diamond

UKURASA 20



**Klopp,** Fabinho wamuita Mbappe

UKURASA 21


## MAISHA

Januari 31, 2021 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



Ukurasa 10

**Udhaifu wa mzazi usipotoshe ukweli**



**MAISHA NI NYUMBA**
Usiichoke nyumba yako, ifanyie utundu uifurahie



**HARUSI**
Ukurasa 12



**UNGA WA RIWA**
**Hupamba ngozi laini inayong'aa**
Ukurasa 14

UKURASA 9

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII


Jumapili Januari 31, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0580477
www.ippmedia.com


www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**RIPOTI MAALUM**

# Mambo 6 yanayoponza vijana dawa za kulevya

• **Wafungwa** wanawake waongoza uraibu gerezani ... *Endelea ukurasa 5*

## YALIYOMO


UKURASA WA 3
**BASHIRU AWASHTUKIA WATENDAJI KUFICHA MATATIZO YA WANANCHI**
KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, ameonya tabia...

UKURASA WA 3
**MBARONI KWA TUHUMA UTOROSHAJI WA MIFUGO**
JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na...

UKURASA WA 8
**NAFASI NA WAJIBU WA MUME KATIKA NDOA**
KAMA nilivyoeleza katika makala iliyopita, mpango wa asili wa Mungu...




## Dada wa kazi adaiwa kunyonga mtoto wa bosi wake

UKURASA 2



## JPM aagiza msako wa madaktari waliokimbia ajira serikalini

UKURASA 2




Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store


**MICHEZO** SIMBA, TP MAZEMBE ZAIDI YA FAINALI LEO UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# JPM aagiza msako madaktari waliozikimbia ajira serikalini

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ameagiza madaktari waliohama Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tabora na kukimbilia hospitali binafsi kwa kigezo cha maslahi, wafuatiliwe waliko na hatua zichukuliwe dhidi yao.

Alitoa maagizo hayo jana wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa jengo la wagonjwa wa dharura la Hospitali ya Rufani Mkoa wa Tabora, utakaogharimu Sh. milioni 616.3.

Rais Magufuli alihoji sababu za madaktari hao walioomba kuajiriwa serikalini na kuziba nafasi za wengine.

"Kwa sababu kazi ya udaktari ni kazi ya kumtolea Mungu sadaka, hata wauguzi hakuna anayeridhika na mshahara, kumbe huyo alipofika hapa akaondoka pamoja na mshahara wetu, kwanini asishtakiwe kwa wizi?" alihoji.

Kiongozi huyo wa nchi alipewa taarifa kuwa hospitali hiyo ina madaktari bingwa watano na walioondoka mpaka sasa ni watatu.

"Walisomeshwa na serikali? Warudishe hizo fedha, watafutwe ili kujua fedha zetu zipo wapi? Kwa sababu hakuna anayeridhika na mshahara, hata mimi siridhiki nao, hata manesi hawaridhiki lakini wanajituma.



Rais Dk. John Magufuli, akimsikiliza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, wakati akikagua ujenzi wa matangi makubwa ya kuhifadhia maji katika mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria katika miji ya Tabora, Igunga na Nzega jana. **PICHA: IKULU.**

"Tunataka wote matatizo yetu tuyatatue kwa pamoja, hatuwezi kuyatatua kwa siku moja, tunafahamu tunachukua hatua nyingi kuimarisha huduma za afya.

"Kulikuwa na upungufu mkubwa wa watumishi wa afya, tumeajiri zaidi ya watumishi wa afya 14,000 katika kipindi cha miaka mitano," alibainisha.

Rais Magufuli alisema mwaka jana, waliajiri watumishi wa afya 1,000 na wamejenga hospitali za wilaya 102, hospitali za rufani tatu na vituo vya afya 487.

"Tulianza na hizo na baadaye tunaingia kwenye maslahi ya watumishi wa afya, tunajua wanafanya kazi kubwa ya kujitolea, ninawapongeza sana, mbona wewe hujakimbia? Kinachohitajika ni uzalendo.

"Wanawake wanaumwa, wengine wanatakiwa kufanyiwa upasuaji, wewe unakimbia, mfuatilie huyo daktari aliyekimbia hapa na uifuatilie na hiyo hospitali ikiwezekana tunamfungia daktari na kuifungia hospitali aliyokwenda huko, ili watu wajifunze kwamba Wizara ya Afya siyo ya kuchezewa tu.

"Mtu anasomeshwa kwa fedha za watu maskini na wanapata mkopo kwa asilimia 100, halafu wanamaliza wanakimbia maslahi madogo.

"Si ungekimbia wakati unasoma. Fedha yetu umekula halafu unasema maslahi madogo, tunataka maslahi yaboreshwe, ila lazima tuanze na kimoja, huwezi kuboresha maslahi wakati hata hospitali huna, vifaa huna," alisema.

Rais Magufuli alisema suala la maslahi ya watumishi wanaliangalia kikamilifu kulingana na bajeti inavyokwenda.

"Wahudumu wa afya uzalendo unatakiwa kuwa mbele, nimesikia changamoto ya jengo hapa, nitazungumza na Waziri na TAMISEMI tuone namna ya kusaidia," alisema.

Rais Magufuli alisema ameambiwa kwa sasa hospitali hiyo ina chumba kimoja cha kuhudumia wagonjwa wa dharura ilhali kila siku wanapokea wastani wa wagonjwa 15 wa kundi hilo.

"Jengo hili lenye uwezo wa kupokea wagonjwa wa dharura 50 litaokoa maisha ya wananchi wa Tabora, mradi huu umefadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Afya (Global Fund), tunawashukuru kwa ufadhili huu," alisifu.

Akizindua miradi ya maji iliyotekelezwa mkoani humo, Rais Magufuli alisema hadi sasa vipo vituo 728.

"Kwa kazi hii ninawapongeza makandarasi na wahandisi na kabla sijasahau waziri alitoa ombi la mhandisi ambaye muda wa kustaafu umefika na kuomba aongezwe muda. Kwa kazi hii mliyofanya, ninamwongezea miaka miwili," alisema.

Rais Magufuli alisema fedha za utekelezaji mradi huo ni za mkopo kutoka Benki ya Exim ya India na kwamba ulianza Agosti 2017 na kukamilika Februari mwaka jana na sasa wako katika kipindi cha uangalizi kitakachokamilika mwezi ujao.

Alisema Serikali ya India ilitoa mkopo mwingine kwa Tanzania wa kutekeleza mradi wa maji Mlandizi, Kibamba, Lindi na Chalinze na kutoa Dola za Marekani milioni 500 (sawa na Sh. trilioni 1.2) ili kutekeleza miradi ya maji kwenye miji 28 pamoja na Zanzibar.

Alisema 2015 wakati wa kugombea Urais, wabunge wa Tabora walisema mkoa huo umesahaulika ndiyo maana aliagiza Sh. bilioni 617 zipelekwe ili kutekeleza miradi ya maji.

"Ninakuagiza Waziri wa Maji, hakikisheni wananchi wanapata maji, siyo maji yanabaki kwenye matenki, nimeagiza!

"Pia, ninataka maji haya yaliyofika Tabora, yafike Urambo, Sikonge na Kaliua, bahati nzuri zipo Sh. bilioni 25 zilizookolewa, zikatumike kutekeleza miradi kwenye hizo wilaya tatu," aliagiza.

Aliipongeza Wizara ya Maji kwa utekelezaji huo na kuwaeleza kuwa awali, miradi mingi ilikuwa ikisuasua na sasa wameanza na mwelekeo wa kuhakikisha wananchi wanapata maji kwa asilimia 85 vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2025.

Rais Magufuli alisema tatizo kubwa la Mkoa wa Tabora analoliona ni majungu mengi, akionya kuwa hayajengi na kuwataka viongozi waliopewa madaraka, wajenge umoja.

"Mwenyekiti wa maadili ya wabunge ni huyu hapa, lakini Tabora anapigwa vita, hamuwezi mkawa wabunge wote, uchaguzi umekwisha na mbunge ni Mwakasaka, umtake usimtake, Mwakasaka ataendelea kusaka miaka mitano.

"Kikubwa ni yale majungu majungu, mlinichagua niseme ukweli wa Mungu ndiyo maana ninasema hapa mbele yenu, ninajua na mimi siyo ajabu nikitoka hapa nitapigwa majungu, mpige litavunjika huko, ninaendelea kwenda mbele," alisema.

# Dada wa kazi atuhumiwa kunyonga mtoto wa bosi

**Na Halfani Chusi**

JESHI la Polisi linamsaka mfanyakazi wa ndani, ambaye utambulisho wake wa majina una utata, kwa tuhuma za kumuua mtoto wa bosi wake kwa kumnyonga.

Hidaya Ali, mkazi wa Kawe Mzimuni jijini Dara es Salaam ambaye ni mama wa mtoto anayedaiwa kuuawa kwa kunyongwa, alisema tukio hilo lilitokea Jumatano nyumbani kwake.

Alisema kuwa mtoto wake wa kike mwenye umri wa miezi 10, aliuawa kwa kunyongwa na mfanyakazi wake huyo kisha kutoweka nyumbani.

"Siku ambayo mwanangu alinyongwa na kufa, niliamka asubuhi na dada wa kazi tukaenda sokoni kununua vifaa vya nyumbani ili tupike kabisa chakula niwaache na chakula kabla sijaenda kazini.

"Mimi huwa ninaondoka saa tano mchana na kurudi saa tano usiku, lakini kwa bahati mbaya tulichelewa kurudi sokoni, hivyo nikashindwa kuwapikia chakula.

"Nikamuachia pesa ya matumizi mfanyakazi wangu ale kwa kuwa mtoto alikuwa amekunywa uji. Baada ya hapo, nikaondoka kuelekea kazini.

"Ilipofika saa mbili usiku, nikapiga simu nyumbani kuongea na dada wa kazi ili kujua wanaendeleaje na mwanangu akapokea simu huku nikisikia sauti ya mwanangu kwa mbali analia, nikamuuliza 'mbona mtoto analia?'

"Dada akanijibu 'anataka kulala ndiyo maana analia, siunajua huyu akitaka kulala, lazima alie kwanza', nikamwambia sawa mbembeleze alale.

"Basi tokea hapo sikumpigia tena simu mpaka muda wa kurudi. Wakati wa kurudi, nilipofika nyumbani nikakuta milango yote imerudishiwa na taa zimezimwa, nikaingia sebuleni nikakuta maziwa hayajafunikwa, sebuleni kupo ovyo ovyo.

"Kufungua mlango wa chumbani, ninakuta mwanangu Heleni Chistopher, damu na mapovu vinamtoka hadi vimekauka na yeye akionekana kakabwa shingoni hadi kufa.

"Nilipiga kelele kwa sababu tukio hilo niliona ni la ajabu, watu wakajaa akiwamo mjumbe wa serikali ya mtaa, tukaita polisi kutoka Kituo cha Kawe wakaja kuuchukua mwili na kuupeleka Hospitali ya Lugalo," alisimulia.

Mama huyo alidai kuwa dada huyo alimtoa Morogoro miezi miwili iliyopita, akijitambulisha kwa jina la Lillian na kudai ana umri wa miaka 19, lakini siku chache kabla ya kutokea kwa tukio hilo, alibaini dada huyo ana kitambulisho cha taifa chenye picha yake na jina la Jesca.

Kamanda Polisi Mkoa wa Kinondoni, Ramadhani Kingai, alipotafutwa na Nipashe jana, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

"Baada ya mwili kufika kituo cha polisi, tuliupeleka Hospital ya Lugalo ambako baada ya uchunguzi, daktari alitueleza kuwa mtoto ameuawa kwa kukabwa na kitu shingoni.

"Sasa, Jeshi la Polisi linaendelea na taratibu za kumtafuta mtuhumiwa popote alipo kwa sababu inaonekana baada ya kufanya tukio hilo, alikimbilia kusikojulikana," alisema.

Kamanda huyo alitoa wito kwa wafanyakazi wa ndani kutojichukulia sheria mkononi na badala yake wafike kwenye mamlaka husika kama kuna stahiki hawajatimiziwa. na kodi ya ongezeko la thamani kwa teknolojia inayoingizwa nchini.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Enorck Nyasebwa, alisema timu ya wataalamu itakutana kufutafuta suluhisho la kuongeza uzalishaji nchini.


## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 4 | SKYCITY LIMITED | GARI | TOYOTA HILUX T 956 DKN | J &J RECOVERIES | 14-02-2021 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Taratibu na gharama za kubadili hati miliki kadi ya gari ni juu ya mnunuzi.

HABARI KITAIFA

KIKAO



Waziri wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, akizungumza na wazalishaji wa sukari nchini na kusikiliza kero zao ili kuzitatua na kuongeza uzalishaji wa sukari nchini, kikao hicho kilifanyika jana jijini Dodoma, **PICHA NA MPIGAPICHA WETU**

# Bashiru awashtukia watendaji kuficha matatizo ya wananchi

**Na Enock Charles**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, ameonya tabia ya baadhi ya viongozi nchini, kuficha matatizo halisi ya wananchi pale viongozi wa kitaifa wanapozuru katika maeneo husika.

Amesema kufanya hivyo kunawanyima wananchi haki ya kusikilizwa kero zao na kupata maendeleo.

Dk. Bashiru alitoa onyo hilo juzi, katika ziara yake ya kikazi mkoani Tabora, akisema ili kiongozi atatue tatizo, ni muhimu alione kwa macho yake kuliko ilivyo sasa ambapo baadhi ya viongozi katika mikoa na wilaya wamekuwa na tabia ya kutokuweka wazi baadhi ya kero za wananchi, akitolea mfano matatizo ya barabara na maji.

"Tuache maigizo tunafanya kazi za umma, barabara haipitiki, Rais akija aione kwamba haipitiki.

"Kama hakuna maji, siyo mnakwenda kuunga unga maji ya saa 24, baada ya kuondoka yeye tu, yanakatika," Dk. Bashiru alionya.

"Huyu Rais wetu (Dk. John Magufuli) habadiliki, anataka ukweli na kwa chama chetu, msema kweli ni mpenzi wa Mungu na tuna ahadi inayosema 'nitasema kweli daima, uongo kwangu mwiko," alisema.

Vilevile, Dk. Bashiru aliwataka viongozi wa chama na serikali kufika katika kata na vijiji badala ya kuishia mijini.

Mtendaji huyo wa chama aliwaonya wanaotumia gharama kubwa katika ziara za viongozi huku hali ya wananchi wanaowaongoza ikiwa mbaya.

"Ninawaomba viongozi wa kitaifa na wa mikoa wafanye ziara kwenda chini kwenye matawi na kwenye kata, tuache tabia ya kufanya ziara katika wilaya na mikoa wakati wanachama na uhai wa chama upo katika ngazi ya kata na matawi," alisema.

# Mbaroni kwa tuhuma utoroshaji wa mifugo

**Na Mwandishi wetu, Arusha**

JESHI la Polisi Mkoa wa Arusha kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wamewakamata watuhumiwa watatu wa wizi na utoroshaji wa mifugo maeneo ya mipakani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Polisi Salum Hamduni, jeshi hilo limewakamata watuhumiwa hao katika Tarafa ya Loliondo, Wilaya ya Ngorongoro mkoani huko.

Kukamatwa kwa watuhumiwa hao ni kufuatia agizo alilolitoa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, Jumatano ya wiki iliyopita la kukamatwa kwa watuhumiwa 67 wa utoroshaji wa mifugo na mazao yake.

Kamanda Hamduni alisema kukamatwa kwa watuhumiwa hao watatu ni baada ya kufanyika operesheni ya kudhibiti wizi na utoroshaji wa mifugo hiyo maeneo ya mipakani baada ya kuwapo kwa taarifa za uwapo wa watu wanaojihusisha na wizi na utoroshaji wa mifugo katika Wilaya ya Ngorongoro.

Alisema upelelezi bado unaendelea kuhusiana na tukio hilo na utakapokamilika, jalada litapelekwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria.

Alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanafuata sheria za biashara ya usafirishaji wa mifugo na kwamba wasipofanya hivyo, watakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria.

Waziri Ndaki pia alipokea ripoti ya uchunguzi kutoka kwa jeshi hilo kuhusu utoroshaji wa mifugo ambayo ilibainisha kwamba kabla Novemba 7 mwaka jana, mifugo iliyokuwa inatoka kwenye minada ya awali ya Handeni na Kilindi kuelekea Kenya kupitia Mpaka wa Horohoro, haikuwa inafuata taratibu za forodha kama ilivyo kwa shehena nyingine.

Ripoti hiyo ilibainisha kuwa takwimu za daftari la mifugo katika Mpaka wa Horohoro zinaonyesha idadi ya mifugo iliyopitishwa kwenda Kenya kwa kipindi cha miaka 17 kutoka mwaka 2003 hadi Novemba 2020, ilikuwa ni ng'ombe 24,980 na mbuzi/kondoo 9,368, sawa na wastani wa ng'ombe 122 na mbuzi/kondoo 46 kwa mwezi.

Taarifa hiyo ilibainisha pia kuwa kati ya Novemba 7 hadi Desemba 9 mwaka jana, jumla ya ng'ombe 1,096 na mbuzi/kondoo 1,044 walipitishwa katika kituo cha forodha kwenda Kenya, kiwango ambacho ni wastani wa idadi ya mifugo iliyopita mpakani ndani ya mwezi mmoja kulinganisha na siku za nyuma.

Pia, ilibaini viashiria vya udanganyifu katika kuweka rekodi za mifugo inayokaguliwa kwenda Kenya hususan katika Mpaka wa Hororohoro na Tanga.

# Ofisa Afya kizimbani tuhuma wizi wa fedha

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

ALIYEKUWA Ofisa Afya na Mratibu wa Mradi wa Belgium Fund for Food Security katika Halmashauri ya Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Emanuel Mziwanda (61), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya hiyo kwa tuhuma za kugushi nyaraka na kujipatia Sh. milioni 15.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, taasisi hiyo imemfikisha katika mahakama hiyo juzi kwa tuhuma za kuandaa nyaraka za kuonyesha matumizi ya Sh. milioni 15 kama gharama za kuendesha mafunzo kwa maofisa ugani 60.

Hata hivyo, alisema uchunguzi umeonyesha kwamba mafunzo hayo hayakufanyika na wala maofisa ugani hao hawakulipwa posho hizo, bali mshtakiwa alijipatia kiasi hicho cha fedha kwa njia ya udanganyifu.

Alisema kutokana na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuridhika na ushahidi uliokusanywa, iliruhusu mtuhumiwa kufikishwa mahakamani na kusomewa mashtaka.

Alisema mtuhumiwa huyo alisomewa mashtaka manne, matatu yakiwa ya kutumia nyaraka kumdanganya mwajiri wake kinyume cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

"Kosa lingine ni kusababisha hasara ya Sh. milioni 15 kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 marejeo ya 2002," alisema.

Kibwengo alisema mtuhumiwa huyo amepelekwa rumande kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo wa kutoa dhamana kwa mashtaka husika.

Aliwaasa watumishi wa umma kujiepusha na vitendo vya udanganyifu, ili kutokuwa kikwazo cha maendeleo ya taifa.

RIPOTI MAALUM

# Shule zilivyotelekeza mwongozo wa corona



Mwanafunzi wa Shule ya Msingi Makole akiingia shuleni huku kukiwa hakuna vifaa vya kunawa mikono kwenye shule hiyo.

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

KUNA msemo kwamba 'kinga ni bora kuliko tiba', unaosisitiza umuhimu wa kuchukua tahadhari kujikinga dhidi ya jambo fulani badala ya kusubiri litokee ndipo ulitatue.

Machi 16, mwaka jana, Tanzania iliripoti kuwa na mgonjwa wa kwanza wa corona. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), idadi ya visa iliongezeka kutoka kimoja hadi kufikia 480 Aprili 2020 huku vifo 18 vikiripotiwa kutokana na ugonjwa huo.

Serikali ilichukua hatua mbalimbali kukabiliana na virusi hivyo kuhakikisha inalinda wananchi wake dhidi ya janga hilo.

Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni kutolewa kwa miongozo ya kitaalamu kwa umma kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, ikielekeza jinsi ya kuepuka maambukizi ya ugonjwa huo usio na tiba hadi sasa duniani.

Miongozo iliyotolewa ilielekeza kukaa umbali wa mita moja hadi mbili kati ya mtu na mtu hasa anayekohoa na mwenye historia ya kusafiri kutoka nje ya nchi, kunawa mikono kwa maji safi tiririka na sabuni, kuvaa barakoa na kutumia vitakasa mikono.

Mikusanyiko ya watu nayo ilizuiwa kwa muda, ikiwamo kufungwa kwa shule na vyuo ili kupunguza kasi ya kusambaa kwa ugonjwa huo nchini.

Baada ya ugonjwa huo kudhibitiwa, serikali ilitangaza kufungua shule Juni mwaka jana, huku ikitoa mwongozo uliokuwa ukiainisha mambo mbalimbali ya kufuatwa kwa wanafunzi na walimu ikiwamo kunawa mikono kwa maji safi na sabuni.

Aliyekuwa Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliagiza shule kuwa safi na kutengwa maeneo ya kunawa mikono katika maeneo ya kimkakati.

Baada ya kubainika ugonjwa huo umetokomezwa nchini, mwongozo huo wa kukabiliana na corona kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo shule kwa sasa ni kama umetelekezwa huku wanafunzi wakiingia darasani bila kunawa mikono na maji tiririka.

Nipashe ilifuatilia katika baadhi ya shule za msingi na sekondari jijini Dodoma ikiwamo Shule za Msingi Uhuru, Makole na Sekondari ya Kisasa na kubaini taratibu za kunawa mikono kila wanapoingia na kutoka shule hazifuatwi huku zingine zikiwa na ndoo zisizo na maji.

Mbali na shule, hata wananchi wamepuuza unawaji wa mikono mitaani, licha ya vifaa vya kunawa mikono kuwapo kwenye baadhi ya maeneo.

**KAULI ZA WANANCHI**

Mkazi wa Chang'ombe, Stella John, anasema baada ya kutangazwa ugonjwa wa corona haupo, watu wamepuuza kunawa mikono kwa maji tiririka na wanapokuta yamewekwa, wanapita bila kunawa.

"Wataalamu wa afya wanatuambia tukinawa mikono, inasaidia kupambana na ugonjwa wa corona na magonjwa mengine ya mlipuko, tatizo sisi wananchi hadi tusukumwe kunawa mikono," anasema.

Paul Madeha, anasema hajaona umuhimu wa kunawa mikono kila anapoingia maeneo mbalimbali mitaani kwa kuwa ugonjwa wa corona haupo.

"Kwani ugonjwa umerudi? Kama haupo, kwanini mimi ninawe mikono, yaani tunanawa tu kama tunakula," anasema.

Zawadi Matumbi anasema baada ya kutangaziwa corona imeisha, shule zilianza taratibu kupuuza mwongozo hasa wa unawaji mikono bila kujua hali hiyo inasaidia kuwaepusha watoto dhidi ya magonjwa mengine ikiwamo kipindupindu.

Adamu Ally, anasema ameshuhudia watoto wao hanawi mikono wanapowafikisha kwenye eneo la Shule ya Msingi Kisasa kwa sababu hakuna sehemu iliyoandaliwa kwa ajili hiyo.

Ally anaiomba shule hiyo kuendelea na utaratibu wa kuweka vifaa vya kunawa mikono getini na kwenye vyumba vya madarasa kwa sababu utaratibu huo ulikuwa unasaidia kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa ya homa ya matumbo.

**WALIMU WALONGA**

Mkuu wa Shule ya Sekondari Dodoma, Amani Mfaume, anasema shule yao imeweka vifaa vya kunawa mikono kwa ajili ya kujikinga na magonjwa, lakini wapo wanafunzi na watumishi wanaopuuzia kunawa mikono yao.

Mfaume anasema shule imeweka vifaa vya kunawa mikono nje ya kila chumba cha darasa ili wanafunzi na watumishi wa shule hiyo watumie wakati wowote wakiwa shuleni.

Anataja sababu ya shule hiyo kuendelea na utaratibu wa kunawa mikono wakati wa kuingia na kutoka kuwa ni kujikinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko, hasa yanayotokana na uchafu kwenye mikono ya mtu.

Anasema lengo la shule ni kuendelea kuhakikisha kila siku vifaa hivyo vinakuwa na maji na sabuni ili kuwakinga na magonjwa wanafunzi na watumishi waliopo shuleni.

Mkuu wa shule huyo anasema wageni wanapoingia shuleni, utaratibu wa kufuatwa ni huo, lakini wengine wanapita bila kunawa licha ya vifaa vya kunawa mikono na vitakasa mikono vimewekwa ofisini na getini.

**OFISA AFYA**

Ofisa Afya Jiji la Dodoma, Abdallah Mahia, anasema hana taarifa za shule kupuuza kutekeleza mwongozo wa Wizara ya Afya na kwamba kila shule kuna mwalimu anayeshughulika na masuala ya afya.

"Tangu kipindi kile cha maambukizi ya corona, tuliendelea kuhamasisha kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu kuendelea kunawa mikono ili kuepukana na magonjwa yanayotokana na uchafu kama kipindupindu, minyoo na homa za matumbo.

"Kama kuna shule ambayo imepuuzia haya mambo, nitakuwa nimesikitika sana maana ninachofahamu shule zinaendelea na taratibu za unawaji wa mikono na si kwa sababu tu ya corona.

"Kila shule imepewa vifaa vya kunawa mikono, inawezekana baadhi wamevifungia ndani. Wananchi wengi ukiwaambia mtu unawe mikono na maji tiririka na sabuni, wanauliza kama ugonjwa umerudi," anasema.

Anatoa wito kwa wananchi kujenga utamaduni wa kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono ili kujikinga na magonjwa.

"Kunawa mikono ni msingi wa afya katika jamii, magonjwa mengi yanayoripotiwa kwenye vituo vya kutoa huduma yanatokana na uchafu ni asilimia 80 ya magonjwa yote, mikono yetu ikiendelea kuwa safi, hatutapata magonjwa," anasema.

Anawataka walimu kusimamia ipasavyo watoto kunawa mikono ili kujikinga na maradhi.

Ni takriban mwaka mmoja tangu kuzuka kwa ugonjwa huo Desemba 2019 Wuhan, China ulikoanzia na kuenea kwa kasi duniani.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), zinabainisha kuwa tangu Desemba 2019 hadi Januari 25 mwaka huu, kulikuwa na wagonjwa milioni 99.4 na vifo milioni 2.13 vilivyoripotiwa kutokana na virusi hivyo.

Desemba mwaka jana, Taasisi ya Kuzuia na Kudhibiti Magonjwa Afrika (Afrika CDC), ilinukuliwa ikibainisha kuwa watu milioni 2.25 walipata virusi hivyo na vifo 53,543 vilitokea barani.

Hivi sasa nchi mbalimbali zimeendelea kuchukua hatua ikiwamo kuweka sharti la upimaji maambukizi hayo kwa wasafiri wanaotoka nchi moja kwenda nyingine, Tanzania ikiwamo.

Kwa mujibu wa Afrika CDC, nchi zilizoathiriwa vibaya zaidi ni Afrika Kusini, Morocco, Misri na Ethiopia.

MAKALA MAALUM

# Mambo 6 yanayoponza vijana dawa za kulevya

## ■Wafungwa hatarini zaidi 'ubwiaji unga'
## ■Wanawake waongoza uraibu gerezani

Na Gwamaka Alipipi

DAWA za kulevya zimekuwa janga kwa taifa, kundi linaloathirika zaidi ni vijana wa kiume na kike kunakochangia kupoteza nguvu kazi ya taifa.

Dawa hizo zimekuwa na athari kwa taifa na jamii, kwa kuwa huchangia kuwapo kwa mmomonyoko wa maadili na hudhoofisha nguvu kazi.

Matumizi ya dawa hizo yameendelea kuwa tatizo katika jamii hususan kwa vijana wenye umri kati ya miaka 14-24, wengi wao wakianza kujihusisha na matumizi hayo wakiwa katika shule za msingi na sekondari.

Baa hilo huchochewa na sababu mbalimbali za kifamilia, kijamii na kiuchumi zinazowasukuma vijana kujihusisha na matumizi ya dawa hizo.

Nipashe inazungumza na Kamishna Msaidizi wa Kinga na Tiba wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Dk. Cassian Nyandindi, **(pichani)** kufahamu sababu zinazochangia vijana kujiingiza katika matumizi ya dawa hizo.



Dk. Nyandindi anabainisha kuwapo sababu kuu sita, miongoni mwake ni msukumo rika na kufuata mikumbo, akifafanua kuwa baadhi ya vijana hurubuniwa na kushawishiwa na vijana wenzao wanaotumia dawa hizo.

Anasema tatizo hilo huwapata mara nyingi vijana wenye malezi duni, wenye mazingira magumu na hatarishi ya kuishi kama vile migodini na watoto wa mitaani.

Dk. Nyandindi anasema makundi hayo hujitokeza katika jamii kutokana na sababu mbalimbali za kifamilia ikiwamo kusambaratika kwa familia, malezi mabaya ya wazazi kwa watoto na umaskini.

Sababu nyingine ni hali ya baadhi ya watoto kuishi na ndugu, rafiki, mpenzi au mwenza ambaye anajihusisha na dawa za kulevya.

Anataja sababu nyingine kuwa ni urahisi na upatikanaji dawa za kulevya kama vile bangi na mirungi ambazo hutokana na mimea inayostawi katika maeneo mbalimbali nchini, zimekuwa kishawishi kikubwa kwa vijana wanaotoka maeneo hayo kujiingiza katika utumiaji wa dawa hizo.

Anasema ukosefu wa stadi za maisha na elimu ya kujitegemea kwa vijana pamoja na ukosefu wa ajira nako kumechangia baadhi ya vijana kuingia katika matumizi ya dawa hizo.

Dk. Nyandindi anasema: "Baadhi ya waathirika wa dawa hizo wameingia katika matumizi hayo kutokana na magonjwa ya akili kama vile saikosisi (kuchanganyikiwa), msongo wa mawazo, sonona na kihoro, wamekuwa wakitumia dawa za kulevya kama njia ya kustahimili magonjwa hayo."

Anasema kuongezeka kwa teknolojia za kisasa, utandawazi na mitandao ya kijamii nako kumechangia kwa kiwango kikubwa mmomonyoko wa maadili kwa vijana kwa kuiga maisha, mitindo, mila na desturi za kigeni ikiwamo kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

### WANAWAKE NA 'UNGA'

Dk. Nyandindi anabainisha kuwa wanawake hupata uraibu na madhara mengine yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya kwa haraka zaidi kuliko wanaume.

Anasema utafiti unaonyesha wanawake wengi duniani hutumia dawa tiba zenye asili ya kulevya kama vilevi.

Anasema wanawake walioathirika na dawa hizo hupata uoga kujitokeza kwenye huduma za matibabu ya uraibu kutokana na unyanyapaa, ujauzito au matatizo ya kisheria.

Dk. Nyandindi anasema matumizi ya dawa za kulevya kwa wajawazito husababisha athari kwa watoto wao na wanapojifungua, suala la malezi huwa tatizo pia.

### WAFUNGWA HATARINI

Dk. Nyandindi anasema wafungwa ni kundi la kijamii ambalo liko katika hatari kubwa ya kupata madhara yanayosababishwa na matumizi ya dawa za kulevya bila kuwa na huduma za afya za kutosha.

Anasema watumiaji wengi wa dawa za kulevya hujikuta wakifungwa kutokana na kujihusisha na uhalifu mbalimbali ili kupata fedha za kununua dawa hizo.

Dk. Nyandindi anasema kutokana na mazingira magumu yaliyoko gerezani, wafungwa wengi wanajiingiza kwenye matumizi ya dawa za kulevya ili kukabiliana na mazingira hayo.

"Takwimu zilizopatikana kwenye nchi zinazoendelea, zinaonesha kuwa karibu nusu ya wafungwa wote walikuwa watumiaji wa dawa za kulevya kabla hawajaanza kutumikia vifungo vyao.

"Vilevile, utafiti ulionyesha idadi ya wanawake waliokuwa wanatumia dawa za kulevya ilikuwa kubwa kuliko wanaume.

"Kwani asilimia 51 ya wafungwa wanawake walikuwa wana uraibu wa dawa za kulevya mwaka mmoja kabla ya kifungo kulinganishwa na asilimia 30 ya wanaume.

"Idadi hii ni kubwa ikilinganishwa na watumiaji wanawake na wanaume ambao hawajafungwa," anasema Dk. Nyandindi.

Anabainisha bangi iliongoza kwa matumizi katika wafungwa hao, akieleza kuwa asilimia 10 ya wafungwa walikuwa wanatumia dawa za jamii ya afyuni.

Dk. Nyandindi anasema ilibainika asilimia 10 ya wafungwa walitumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidungana kwamba wanaojidunga dawa za kulevya, wanajiweka katika hatari kubwa ya kuambukizwa Virusi vya Ukimwi (VVU) na virusi vya homa ya ini aina C kuliko wanajamii wengine.

"Hii inatokana na uhaba wa sindano za kujidungia na hivyo sindano moja kutumika kwa watu wengi, hivyo kusababisha maambukizi makubwa ya virusi hivyo kati yao," anafafanua.

Dk. Nyandindi anasema mapitio ya utafiti mbalimbali yanaonyesha maambukizi ya VVU kati ya wafungwa waliojidunga yalikuwa mara sita zaidi na homa ya ini aina C, ikiwa mara nane zaidi ya wafungwa wasiojidunga.

Anasema nchi 56 duniani ziliripoti kutoa huduma ya tiba ya methadone walau kwenye gereza moja mwaka 2017.

"Huduma za udungaji salama kwa wafungwa ni chache sana, ambapo nchi 11 ziliripoti kutoa huduma hizo kwenye walau gereza moja.

"Huduma hiyo iliripotiwa kutokuwapo kabisa kwenye nchi 83. Katika kupunguza maambukizi ya VVU na homa ya ini aina C, huduma hizi mbili inabidi zitolewe kwa pamoja," anasema Dk. Nyandindi.

### UDHIBITI DAWA ZA KULEVYA

Licha ya kuwapo kwa biashara ya dawa za kulevya nchini, Dk. Nyandindi anasema DCEA imekuwa ikipambana na maharamia wanaongiza dawa hizo sambamba na watumiaji.

Dk. Nyandindi anabainisha katika kipindi cha mwaka 2019, Tanzania iliendelea kukabiliwa na uwapo wa dawa za kulevya ambazo zimegawanyika katika makundi mawili za viwandani na shambani.

Anasema dawa za kulevya zinazopatikana nchini huhusisha zinazozalishwa nchini na zile zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

Anafafanua kuwa dawa za kulevya zinazozalishwa nchini ni bangi, mirungi na zinazoingizwa kutoka nje ya nchi ni pamoja na heroin, cocaine, mandrax, morphine na bangi iliyosindikwa.

Anachanganua kwamba katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2019, kulikuwa na makosa 7,921 ya dawa za kulevya nchini.

Kati yake, 503 yalihusu dawa za kulevya za viwandani na makosa 7,418 yalihusu dawa za kulevya za shambani.

Anasema watuhumiwa 578 wa dawa za kulevya za viwandani na watuhumiwa 10,326 wa dawa za kulevya za shambani walikamatwa.

Dk. Nyandindi anabainisha katika kipindi hicho, biashara ya bangi ilifanyika kukinaswa tani 21.16 za dawa hiyo kiasi ambacho ni kidogo kulinganishwa na tani 23.61 zilizokamatwa mwaka 2018.

"Hii inaonesha kuwa juhudi za kupambana na kudhibiti uzalishaji na usambazaji wa dawa hii una mafanikio.

"Pia, takwimu za ukamataji zinaonyesha kuwa idadi ya watuhumiwa waliojihusisha na biashara ya bangi mwaka 2019 ilikuwa 8,865 ambayo ni ndogo zaidi kulinganishwa na watuhumiwa 9,744 waliohusishwa na biashara ya dawa hiyo mwaka 2018." anasema.

Anasema katika kipindi cha mwaka 2019, jumla ya mashamba ya bangi 31 yenye ukubwa wa ekari 22 yakiwa na jumla ya miche ya bangi 1,997, yaliteketezwa huku watuhumiwa 29 wakikamatwa kuhusiana na mashamba hayo.

Dk. Nyandindi anasema kwa mwaka 2019 biashara ya mirungi ilifanyika, tani 9.07 za dawa hizo zikikamatwa.

Kwa mwaka huo, kulikuwa na watuhumiwa 1,170 waliojihusisha na biashara hiyo, ambayo ni idadi ndogo kulinganishwa na idadi ya watuhumiwa katika miaka mitano iliyotangulia.

Anasema kiasi cha mirungi kwa mwaka 2019 kiliongezeka kulinganisha na mwaka 2018 kutokana na kubainika kwa mtandao wa usafirishaji wa dawa hizo kutokea Ethiopia kupitia Tanzania kwenda Ulaya, Marekani na Canada kwa njia ya Posta.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Rai ya polisi wafanyakazi wa ndani ifanyiwe kazi

**KILIO** dhidi ya matukio ya ukatili wa kijinsia kimeendelea kusikika karibu maeneo yote nchini, huku wizara yenye dhamana ya ustawi wa jamii ikitoa maagizo tisa yenye mwelekeo wa kutatua tatizo hilo.

Wakati wizara ikichukua hatua hizo wiki hii, Wilaya ya Kinondoni imeripoti kifo cha mtoto wa miezi 10 anayedaiwa kunyongwa na mfanyakazi wa ndani wakati wazazi wake wakiwa kazini.

Hilo siyo tukio la kwanza linaloligusa kundi la wafanyakazi wa ndani kudaiwa kushiriki kufanya unyama wa aina hiyo dhidi ya watoto wa waajiri wao.

Wapo waliowafungia watoto wa mabosi wao ndani ya jokofu, kuna waliowafungia watoto chumbani na kuwatelekeza na baadhi waliripotiwa 'kutembeza' kichapo kikali dhidi ya watoto na kuwasababishia ulemavu na hata kifo.

Baadhi ya sababu zilizo nyuma ya unyama huo, ni waajiri kutowalipa wafanyakazi hao ujira wao kwa wakati na wengine kulipa kisasi baada ya kuwa wamenyanyaswa na wazazi wa mtoto husika.

Mbali na sababu hizo zinazotawala mazingira ya maslahi kwa wafanyakazi wa ndani na manyanyaso yaliyoambatana na matusi, pia wapo walioripotiwa kufanya unyama dhidi ya watoto kutokana na imani za ushirikina.

Nipashe imekuwa miongoni mwa vyombo vya habari ambavyo kwa muda mrefu vimeripoti matukio hayo, yakiwamo ya wafanyakazi wa ndani kunyanyaswa na waajiri wao kwa kunyimwa chakula, kupigwa na mwisho wa siku vitendo hivyo vinapozidi, wanachukua hatua ya kulipiza visasi vyao dhidi ya watoto wanaopewa kuwalea.

Kutokana na tukio la wiki hii jijini Dar es Salaam, Jeshi la Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, lilitoa wito kwa wasaidizi wa ndani kutojichukulia sheria mkononi na badala yake wafike kwenye mamlaka husika kama kuna stahiki hawajatimiziwa.

Nipashe tunaunga mkono rai hii ya jeshi hilo, tukiamini itakuwa miongoni mwa njia sahihi za kupunguza kama siyo kumaliza kabisa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto vinavyofanywa na wafanyakazi wa ndani katika maeneo mbalimbali nchini.

Tunaamini kwamba kundi hilo likiwasilisha malalamiko yake kwa mamlaka husika kisha mamlaka hizo zikachukua hatua stahiki dhidi ya wanaoendekeza ukatili dhidi ya wafanyakazi wa ndani, kutawanusuru watoto wengi dhidi ya unyama huo.

Nipashe tunawakumbusha wafanyakazi wa ndani kwamba ukatili dhidi ya watoto ni kosa kisheria na ni kinyume cha haki za binadamu, hivyo badala ya kulipa kisasi kwa mtoto dhidi ya madhila wanayotendwa na wazazi, wawasilishe malalamiko yao kwa vyombo husika kama ilivyoshauriwa na Jeshi la Polisi Kinondoni.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Msimu huu wakulima wa pamba wanabebwa hivi

Na Sabato Kasika

**PAMBA** ni moja ya mazao matano ya kimkakati, ambayo serikali imeamua kuyawekea mkazo maalum wa kuyaendeleza na pia kuyatafutia masomo ili wakulima wanuifake nayo huku yenyewe ikipata kodi.

Mazao mengine ni korosho, kahawa, chai na tumbaku na sasa yameongezeka mkonge na mchikichi ili kuongeza mapato ya wakulima na kuwa chanzo cha kuaminika cha malighafi katika uchumi wa viwanda.

Lakini kwa muda mrefu, wakulima wa pamba wamekuwa na malalamiko mbalimbali ikiwamo kutolipwa fedha kwa wakati na mizani ya kupima zao hilo kuchakuliwa na kuwaibia.

Malalamiko mengine ni kuuziwa mbolea feki na pia kukatwa fedha mara ya kuuza pamba ili kulipia pembejeo zote ambazo hukopeshwa wakati wanapoandaa mashamba hadi kuvuna.

Katika jitihada za serikali za kuwapunguzia kero wakulima wa zao hilo, iliamua kutopanga bei ya pamba katika msimu wa mwaka 2020 ili kuwezesha soko kuamua na mkulima kupata soko la uhakika.

Badala yake yenyewe ndiyo ikawa msimamizi mkuu kuhakikisha maslahi ya wakulima wa pamba yanalindwa muda wote, wapate soko la uhakika kwa kuzingatia ushindani ili wapate faida.

Hatua hiyo ya serikali ni kutaka kufanya kilimo kuwa cha kibiashara na si cha kujikimu na kuwaondolea wakulima vikwazo ambavyo vinaweza kukwamisha juhudi zao za kuendeleza zao hao.

Aidha, serikali inataka kuhakikisha pamba yote ya wakulima inaongezwa thamani kwa kutumia viwanda vya ndani, hasa pale wafanyabiashara wengi wanapojitokeza kununua pamba yote.

Wakati hayo yakiendelea, wakulima hao wametangaziwa tena habari njema ambayo huenda wakaondokana na malalamiko, kutokana na serikali kusema, haitawakata fedha za mbegu na viuatilifu, msimu wa mwaka 2020/21.

Wakulima ambao wamekopeshwa viuatilifu, hawatakatwa fedha wakati wa kuuza pamba yao, kama ambavyo imezoeleka, kwa kuwa serikali itatumia utaratibu mwingine, ambao haumwumizi mkulima.

Hiyo inaweza kuwa habari njema wanayotangaziwa wakulima wa zao hilo na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussen Bashe katika kikao cha wadau wa pamba, mjini Bariadi mkoani Simiyu.

Uamuzi huo uliotangazwa na serikali unaweza kuwa moja ya mikakati yake ya kuendeleza kilimo na mazao hayo ya kimkakati ya biashara, hivyo wakulima hawana budi kuchangamkia fursa hiyo.

Wakulima wa pamba an hata wa mazao mengine ya kimkakati hawana budi kuchangamkia fursa hiyo, kwa kuwa yanatarajiwa kuendelea kuwa chanzo kikuu cha ajira na fedha za kigeni.

Si hapo tu bali serikali inasema, yatakuwa yanauzwa kwa njia ya ushindani huku wakulima wanaozalisha kwa ubora wakinufaika na bei ya juu zaidi kwa lengo la kumwinua mkulima.

Serikali pia inasema, imepanga kuongeza usimamizi katika uzalishaji wa mazao hayo makuu ya biashara, kwa vile kwa kipindi kirefu uzalishaji ulishuka kutokana na matatizo mbalimbali.

Miongoni mwa matatizo yanayotajwa kuchangia hali hiyo, ni kupungua tija katika uzalishaji, baadhi ya wakulima kuacha kulima mazao hayo kutokana na kukata tamaa kwa sababu mbalimbali.

Baadhi ya sababu hizo ni viongozi wa vyama vya ushirika kutotekeleza vyema wajibu wao, wizi, dhuluma na pia ushiriki mdogo wa maofisa kilimo katika kusimamia kilimo cha kitaalamu.

Ni vyema sasa kama vyama vya ushirika vimeimarika, basi wakulima wakumbushwe kuuza pamba kupitia vyama hivyo ili kupunguza ulaghai kwenye mizani kwa kuwa wasimamizi na watumiaji wa mizani watakuwa ni wakulima wenyewe wa pamba na si mawakala.

Hivyo wote wa kilimo wakimo Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA), waanze kutoa elimu kwa wakulima kuhusu kutambua mizani feki na kuihakiki kabla ya msimu wa mwaka huu utakapowadia.

Elimu hiyo inaweza kuwasaidia kujilinda wenyewe wakati maofisa vipimo wanapokuwa hawapo katika vituo vya kuuzia pamba yao, na pia ni kuwawezesha kupata faida ya thamani kamili ya jasho lao.

Kwa mikakati hiyo na mingine mingi, ni wazi kwamba, pamba ya Tanzania itarejesha hadhi yake ya kuitwa 'dhahabu nyeupe' na kuweza kutumika katika uimarishaji uchumi wa mkulima na nchi kwa ujumla.

**SAFU**

## FIKRA MBADALA



**Nkwazi Mhango, Canada**

# Tuwachunguze watumishi wetu kwenye maeneo yenye mshiko

WIKI iliyopita, tuliahidi kudurusu kwa kina suala la kuchunguzana ili kubana wale wanaoibia umma kwenye nafasi walizopewa kuutumikia na si kuhujumu au kuutumia.

Leo tutaangazia baadhi maeneo yanayopaswa kutushughulisha katika kuchunguzana ili kubaini na kukomesha wizi ambao, kwa nchi nyingi za kiafrika, umekuwa kama desturi kama siyo mazoea tena mabaya ya kimfumo yanayoonekana kukubalika.

Tuanze na bandari. Hili ndilo lango kuu la kutolea na kuingizia bidhaa kwa taifa na mataifa jirani yasiyo na bandari linalopaswa kuchangia pakubwa pato la taifa na si la watu binafsi wachache, yaani wafanyakazi na wateja wao wasio waaminifu na wazalendo yaani wafanyabiashara wanaoshirikiana nao kuhujumu taifa. Hakuna ubishi. Watumishi wengi wa idara hii wana ukwasi usiolingana na kipato chao stahiki japo si wote. Ila ikilinganishwa na wengine si haba.

Ukiondoa bandari, iko Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ambayo nayo licha ya kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na bandari, pia husimamia mapato yote ya taifa.

Pia ina uhusiano wa moja kwa moja na wafanyabiashara wote nchini hivyo kuingiza wizara ya biashara. Wafanyakazi wa idara hii nao ni wa kuchunguza sana tena mara kwa mara. Rejea mkutano wa Rais John Magufuli na wafanyabiashara Ikulu mwaka 2019. Mfanyabiashara mmoja toka Mbeya alisema wazi kuwa wafanyabiashara wengi hutoa rushwa kutokana na baadhi ya maofisa wa TRA kujenga mazingira ya kufanya hivyo kwa kuwakadiria kodi kubwa kuliko stahiki.

Sambamba na bandari ni idara ya biashara ambayo nayo ina ushawishi mkubwa katika kuingiza na kuuza bidhaa nje. Wafanyakazi wa idara hizi nao wana ukwasi usio wa kawaida. Hivyo, nao ni wa kuwekwa kwenye kundi la kuchunguzwa vikali. Je, mchezo huu umeacha? Je, ni wangapi wameutumia kutajirika waliopo na waliokwishastaafu? Je, hawa si wa kufuatilia na kuhakiki mali zao hata kama hawamo kazini tena?

Eneo lingine tunayopaswa kulitupia jicho kali ni Idara ya Uhamiaji. Hii hughulika na utoaji vibali kwa wageni vya kazi na ukazi kwa wageni na pasi za kusafiria kwa watu wetu. Huku nako kuna kila aina ya ulaji ambao huikosesha serikali mapato.

Kuna kipindi pasi zetu zilikuwa zikiuzwa kwa wageni na wahamiaji haramu kama njugu hadi baadhi ya nchi zikaiona pasi yetu kama karatasi isiyo na thamani. Sambamba ni hii ni vituo vya mipakani na viwanja vya ndege ambavyo vilisifika kwa kupitisha madawa na vitu vingine haramu kama ilivyowahi kutokea kupitisha twiga mzima kwenda ughaibuni. Sijui kesi hii imeishia wapi.

Ukiachana na uhamiaji na vituo vya mipakani, kunafuatia mbuga zetu za wanyama na utalii kwa ujumla. Rais Magufuli ni shahidi kuwa kuna watu wamekuwa wakitumia rasilimali zetu kujineemesha wakati taifa likiendelea kuwa maskini. Rais aliwahi kuelezea hoteli moja inayotosha mamia ya dola kulala usiku mmoja ukiachia mbali vitalu vya uwindaji na ujangili ambavyo vina baraka za watumishi wa umma wanaovitumia kujineemesha binafsi.

Linalofuatia ni eneo linaloshughulikia madini. Nchi yetu imejaliwa wingi wa madini ambayo mchango wake ungekuwa mkubwa kwa uchumi wa taifa kama tungepambana na watumishi wabovu kwenye eneo hili na kuyatumia vizuri na vilivyo. Hapa hujagusia kwenye nishati ambapo ulanguzi wa umeme umekuwa kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya watu wetu. Wafanyakazi wa maeneo haya wanabidi kuchunguzwa bila huruma sawa na watajwa hapo juu.

Maeneo mengine yanayopaswa kuchunguzwa bila huruma ni kuanzia Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa (TAKUKURU), mahakama, polisi, Bohari

Kuu ya Dawa na hospitali zetu. Kuna haja ya Rais kuunda kikosi cha siri ambacho kitakuwa kikiwachunguza hata wale tuliwaamini kuwachunguza wengine.

Leo nimegusia maeneo husika kwa kuangalia uzoefu wangu hapa Kanada na nchi nyingine tunazoiita zilizoendelea ambazo hazina mchezo na mapato ya serikali na yale ya wananchi au wakazi wake kama sisi. Kila mwananchi na mkazi lazima ajaze taarifa za kodi na mapato yake kila mwaka kwa mujibu wa sheria na siyo utashi.

Ukiwa na pesa zaidi ya kipato chako bila maelezo, inataifisha na unashitakiwa kwa makosa ya jinai. Hii ndiyo siri kubwa ya utajiri wa nchi husika pamoja na mengine.

Mwisho, serikali yetu inapaswa kuanzisha mfumo ambapo kodi yake nyingi hukusanywa toka kwenye bidhaa na huduma moja kwa moja. Kwa mfano, hapa Kanada kuna aina mbili kwenye bidhaa na huduma. Kodi ya serikali kuu na ile ya serikali ya mkoa. Unaponunua kitu au kupewa huduma, serikali hupata pesa yake hapo hapo.

Kufanikisha hili, kila anayeuza au kutoa huduma lazima atoe risiti. Pia lazima awe na mashine ya kielektroniki (EFD) kwenye biashara yake. Kutoa EFD si jibu kama hakutakuwa na mfumo endelevu, madhubuti na wa uhakika wa kuhakikisha hazichezewi au kutotumika.

Hivyo, lazima kuwe na sheria kali ya matumizi ya mashine hizi. Muhimu, kuwachunguza watumishi kwenye maeneo yanaoingiza au kuhusika na mshiko lazima kuwe endelevu. Wanaogundulika waadhibiwe vikali ili kuwaonya wengine. Kati ya yote, ni kubana fursa yoyote ya mtu kuwa na utajiri usio na maelezo.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO



**Na Joseph Kulangwa**

# Tusiteketeze kila tukamatacho jana

BODI ya Kusimamia Michezo ya Kubahatisha nchini (GBT), mkoani Singida, imeteketeza mashine 13 za mchezo wa kubahatisha, zilizokamatwa baada ya kubainika ziliingizwa nchini kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za mchezo huo.

Huu ni miongoni mwa michezo ambayo wengine wamekuwa wakiita kamari, na hata wakati mwingine kupigwa marufuku kwa kuwa haramu na wabainikao kuicheza, huchukuliwa hatua kwa kuvunja sheria.

Safi sana, kwamba mashine hizi zimekamatwa baada ya kuingizwa nchini kinyume na taratibu, pengine na kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi ambayo ingelipwa kama hazikupita njia za panya.

Inanikumbusha mwaka fulani maeneo ya Arusha, ambako vifaranga kadhaa vilikamatwa na kuteketezwa moto, baada ya kuingizwa nchini bila taratibu kutoka nchi jirani.

Hatua kama hii pia inaweza kuchukuliwa kwa chakula kinachoingizwa nchini kwa njia hiyo hiyo, au hata bidhaa yoyote inayokiuka sheria, kanuni na taratibu na kukanyaga ardhi ya Tanzania.

Safi kabisa, tunaheshimu taratibu, kanuni na sheria tulizojitungia wenyewe, hakuna wa kulaumu au kulalamikiwa hapo. Unajua kabisa sheria, kanuni na taratibu zipo, wewe kwa makusudi yako unakiuka! Kwa nini visiteketezwe!

Mpaka sasa tunaamini na kujiaminisha, kwamba hatua hiyo ya kuchoma moto bidhaa hizo ndiyo komesha na yenye tija na ni onyo kwa yeyote mwenye nia ya kufanya hivyo. Akiona moto unaviwaka, hatathubutu tena kufanya hivyo.

Naamini adhabu hii inayotolewa kwa bidhaa hizo, zikiwamo mashine na hata wale vifaranga, inavihusu hivyo na bado wamiliki wao nao watakumbana na adhabu stahiki yao, kwa kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Lakini najiuliza, hivi ni kweli kuna tija katika kuteketeza mali hizi au kulikuwa na tija kuteketeza vifaranga wale? Hivi mathalan, wahusika wangechukuliwa hatua kwa ukaidi wao, na mashine hizi wakarudishiwa au la, zikapigwa mnada kingeharibika nini?

Eti, hivi kama mmiliki wa vifaranga wale angechukuliwa hatua na viumbe hao wakaachwa waendelee kukua kwa maslahi yake, au ya wengine hata kama ya watoto yatima, nini kingeharibika?

Hivi mnadhani ni kwa nini JPM amekataa katukatu kusaini wauaji walio magerezani kunyongwa? Anajua kwamba haina tija kuua walioua, kwa sababu ukiwaua waliouawa hawawezi kufufuka.

Lakini mbali na ucha Mungu wake na hofu aliyonayo kwa Maulana wake, anajua akiwanyonga atakuwa amepunguza tu nguvukazi ya Taifa na uzalishaji magerezani utapungua. Kwa nini asiwaache waendelee kulima maisha yao yote na kujilisha, kutulisha na kulisha Taifa!

Tufike mahali tuone ni kipi bora, kwa sababu kupanga ni kuchagua, kama ambavyo tunapokamata magari yaliyofanya makosa ya ama kuingia nchini kipanyapanya au kuingiza magendo, mbona hatuyachomi moto.

Yakikamatwa, tumeshasikia ama yakiuzwa kwa mnada au zikipewa taasisi husika za usalama, kuyatumia kwa kazi zingine. Kwa nini sasa tuteketeze mashine ambazo zingeweza kutuingizia kipato sisi na Taifa? Kwa nini tuchome moto vifaranga masikini wale, badala ya kuwakuza tuwalie mayai au nyama yao?

Wakati mwingine yatupasa kukaa na kufikiria tu kwamba, angalia, tumekamata pombe kutoka nje ya nchi, imeingia hapa kwa njia ya panya na haiji kumwagilia mimea bali kuuzwa na kunywewa.

Pombe hii tuliyoikamata, kwanza si haramu, tumeipima haina sumu na ikinywewa na Watanzania itawachangamsha, lakini pia itaingiza chochote kwenye fuko la Serikali na chochote hicho kitatumika kutekelezea miradi yetu.

Ona, tuna upungufu wa madarasa na madawati, kutwa kucha tunakimbizana kuhakikisha madarasa yanajengwa na madawati yananunuliwa, ili vitoto visome vimekaa kwenye madawati raha mustarehe, havichomwi jua havinyeshewi mvua wala havijikung'uti mavumbi. Tutajenga na nini kama tutaendelea kuteketeza mashine na vifaranga?

Lakini tukumbuke pia, mashine hizo za michezo ya kubahatisha ni ajira kwa vijana wetu ambao hivi sasa wanasoma wanamaliza shule na vyuo na kurudi kwa baba na mama zao wawatafutie ajira.

Hivyo basi wakijitafutia waachwe watafute, wakikosea wakadakwa wamekiuka waadhibiwe lakini wasiteketezewe mitaji yao, kwa sababu baada ya hapo wataanza tena msako wa mitaji, wakiikosa watajiingiza kwenye uhalifu. Nani atalaumiwa sasa? Alamsiki!

## KONA YA UKWELI

# Mitano tena ya JPM katika vita kali ya kuondokana na utegemezi



Na Thobias Mwanakatwe

MIAKA mitano ya utawala wa Rais John Magufuli na mitano mingine aliyoanza nayo Novemba, mwaka jana, ni wazi kuwa mipango yake mikuu ni kuifanya Tanzania kuwa taifa linalojitegemea na si tegemezi.

Dalili zinajionyesha wazi kwamba mwamba huyu JPM hataki utani, amedhamiria kufanya kweli ndiyo maana kuna miradi mikubwa iliyojengwa na inayoendelea kujengwa ambayo inatekelezwa kwa fedha za ndani.

Kubwa ambalo liliwaacha midomo wazi wafadhili ni hatua ya JPM alipoamua Tanzania kugharimia uchaguzi mkuu kwa mabilioni ya fedha wakati katika uchaguzi wowote tumezoa wafadhili wakitupiga tafu. Safari hii JPM kasema tupambane wenyewe. Ni kutokana na misimamo hiyo ya JPM ya kutaka Tanzania isimame kwa miguu yake ndipo tunaposema uhuru wa kweli wa taifa hili unakuja.

Naomba nieleweke ninaposema uhuru wa kweli unakuja simaanishi kwamba Tanzania bado hatuna uhuru, bali nachokimaanisha ni kwamba unapokuwa tegemezi kwa mtu au nchi fulani unakosa uhuru wa kujiamulia mambo yako mwenyewe kwa sababu yule aliyekusapoti au kukupiga tafu atataka ufanye mambo anayoyapenda yeye na huko ndiko kukosa uhuru wa kweli.

Uhuru wa kweli kwa taifa lolote unatafsiriwa katika uwezo wake husika kutambua changamoto za watu wake na kuzitafutia majibu bila msaada kutoka nje au kwa jirani. Taifa linapokuwa halina uwezo wa kutatua matatizo yake ya ndani mpaka lipate msaada toka nje, linaitwa taifa tegemezi na kamwe haliwezi kuwa huru.

Lakini pia hii haina maana kuwa kila taifa lazima liwe na uwezo wa kila kitu na uwezo wa kutatua changamoto zake za ndani bila kutegemea taifa lingine! Hali ya kutegemeana haiepukiki katika dunia ya utandawazi na katika kutatuta Maendeleo ya kweli.

Moja ni uwezo wa nchi husika kiuchumi kwa maana ya uwezo wa kuzalisha bidhaa na huduma na kuziuza ndani na nje ya mipaka yake, hii ndiyo ishara ya kwanza ya uhuru wa taifa.

Pili ni uwezo wa Nchi husika kuendesha mipango yake na mambo yake ya ndani kwa kutumia mapato yake yake ya ndani, hii utafsiriwa kama nchi huru. Uwezo wa kukusanya na kugawanya mapato ya serikali kwenda katika shughuli za maendeleo ni kipimo kizuri cha uhuru.

Tatu ni uwezo wa nchi husika kupunguza utegemezi wa misaada ya kifedha, kiteknolojia na kielimu, pia ni ishara ya uhuru wa kweli katika taifa. Nne, uhuru wa nchi upo katika kudumisha utamaduni wake dhidi ya utamaduni wa nchi zingine na daima taifa usimama kutetea "tunu" zake kama utu, lugha, mavazi, miiko, desturi na utamaduni kwa ujumla.

Uhuru wa bendera au wa kisiasa bila uhuru wa kiuchumi ni kazi bure kwa hiyo taifa linapaswa kuutafuta uhuru wa kiuchumi kwanza kwa gharama yoyote.

Japo kumekuwa na juhudi za makusudi katika awamu zote za uongozi wa taifa la Tanzania katika kuutafuta uhuru wa kiuchumi, awamu ya tano imejipambanua chini ya JPM kwamba inataka Tanzania kuwa mbia wa maendeleo na si tegemezi wa maendeleo.

Juhudi za wazi za kujitegemea za serikali kupitia ukusanyaji wa mapato na ujenzi wa miradi ya kimkakati ni ishara ya kuonyesha taifa linautafuta uhuru wa kweli, yaani uhuru wa kiuchumi.

JPM ameendelea kutafuta maslahi ya kiuchumi ya Tanzania dhidi ya wawekezaji kwa staili ya "Win - Win Situation" kwa kufanya majadiliano mapya katika baadhi ya maeneo ambayo yalionekana tunapunjwa katika sekta ya madini.

Hatua za makusudi za kulinda rasilimali za taifa zimeonekana kuzaa matunda katika maeneo ya rasilimali madini ya tanzanite, wanyamapori, matumizi sahihi ya mapato ya serikali na kadhalika.

Katika kukuza na kuendeleza utamaduni wa taifa, hatua mbalimbali za makusudi za kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya kiofisi katika ukanda wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) zimechukuliwa.

Kuna nia ya dhati kabisa kila mtu anaona ya kuutafuta uhuru wa kweli wa kiuchumi chini ya serikali ya awamu ya tano na matokeo yake yameonekana wazi kwa Tanzania kufikia uchumi wa kati kabla ya kufikia muda kikomo iliyojiwekea.

Hata hivyo, mipango ya serikali ni kama imeanza kuwatisha mabeberu wa ndani na wa nje, hivyo kuwapo kwa vita vya wazi vya kutukwamisha kutufanya tusifikie ndoto yetu ya kuwa taifa huru kiuchumi, hivyo kuwa Taifa kubwa kisiasa.

Kama mipango na hatua zinazochukuliwa na serikali ya awamu ya tano zitafanikiwa basi Tanzania itakuwa miongoni mwa mataifa yenye uchumi mkubwa katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, hivyo kuwa na uwezo wa kujiamulia mambo yake.

Uchumi mkubwa utatupa Uhuru wa kutengeneza ajira na miradi mengine ya kijamii kuwahudumia wazee na Watanzania kwa ujumla kupitia miradi ya afya, makazi na nyanja zingine za maendeleo yao.

Hatua ambazo zinachukuliwa na serikali ya awamu ya tano zinaonyesha wazi kuwa serikali ina kitu inakitafuta kufikia malengo makubwa ya kuwa nchi inayojitegemea na si tegemezi. Shime Watanzania tumuunge mkono JPM.

***MUNGU IBARIKI TANZANIA***

***Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com***

## DARASA LA NDOA

# Nafasi na wajibu wa mume katika ndoa



Na Mch. Dk. Enock Mlyuka

KAMA nilivyoeleza katika makala iliyopita, mpango wa asili wa Mungu kuhusu ndoa ni mume na mke waishi pamoja katika amani na utulivu kamili. Mungu aliwaumba mwanamume na mwanamke ili wahitajiane kwani kila mmoja anacho cha kuchangia katika uhusiano na maisha yao. Mwanamume na mwanamke wanategemeana.

Pamoja kwamba wajibu na majukumu yao yanatofautiana, wako sawa kwa umuhimu. Wote ni watu muhimu katika kujenga familia na jamii iliyo bora.

Wanandoa wakiishi maisha ya kuhitajiana na kutegemeana, pendo la ndoa litadumu. Makala iliyopita nilijadili nafasi na wajibu wa mke katika ndoa. leo, tutaangalia nafasi na wajibu wa mume katika ndoa.

Yafuatayo ni majukumu ya mume katika ndoa:

**Kuongoza na kuelekeza**

Baba ni kiongozi mkuu wa familia na si mtawala wa mke wake, kiasi cha kumnyima fursa ya kutoa maoni, ushauri, kushiriki katika uamuzi na kadhalika. Kinababa wanatazamiwa kuwa na uwezo wa kuongoza familia zao.

Kinababa wanaposhindwa kuongoza familia zao, wasaidizi wao ambao ni wake zao watalazimika kubeba majukumu yao. Majukumu yao yanapobebwa na wake zao wasilalamike na kunung'unika kwani mwanamke anayejitambua hawezi kukubali familia iangamie. Wanawake wana uwezo mkubwa wa kuleta mabadiliko katika maisha ya wengi wakipewa nafasi na kutumika vizuri.

**Kumpenda mke**

Wanawake huongozwa na hisia zaidi. Hivyo, Mungu amempa mume wajibu wa kumpenda mke wake. Waume wanaojua kupenda na kuishi na wake zao vizuri, hunufaika na mema ya mke. Ni vizuri waume wafahamu kwamba, kinachomfanya mke afurahie ndoa yake ni kupendwa kwani upendo ni dai la msingi katika ulimwengu wa mwanamke. Mume anayempenda mke wake hawezi kumfanyia vitendo vya ukatili.

**Kuilinda familia**

Familia hujisikia salama kwa uwapo wa baba. Baba awe muunganishi wa familia yake na si mvurugaji. Anapaswa ailinde familia yake kwa kutoa maelekezo na miongozo bora ya kujenga nidhamu na kuimarisha familia. Pia atengeneze mfumo imara wa kuisimamia familia yake dhidi ya watu waovu na wenye nia mbaya.

**Kutunza na kutoa mahitaji**

Kinachomfanya mwanamume aitwe baba si mtoto au watoto, bali ni majukumu aliyoyabeba katika familia yake kwani wenye watoto huwatunza. Wasiowatunza watoto wao wamepoteza sifa ya kuwa baba, hivyo wamebaki na sifa ya kuwa wanaume tu.

Kwa mantiki hiyo, kutunza familia ni wajibu wa msingi wa baba. Baba anao wajibu asilia wa kuitunza familia yake kwa kuijali, kuithamini na kutoa mahitaji. Baba anapotimiza wajibu huu kwa familia yake, anaongeza thamani ya uwepo wake katika familia.

**Kuwa na muda na familia**

Imejitokeza mahali pengi kuwa mwanamume kaoa, lakini haonekani nyumbani kwake. Hali hii imesababisha watoto wengi leo kuwa na malezi ya mama zaidi kuliko baba. Kinababa wengi hawana muda na familia zao kwa kisingizio cha kazi na kutafuta maisha.

Matokeo yake, watoto wanajengewa mazingira ya kuona mama yao niwa muhimu na thamani zaidi kuliko baba yao kwa sababu ndiye mwenye muda na wao. Hali hii imewaathiri wababa wengi, hasa pale watoto wanapokuwa watu wazima kwani wanamjali zaidi mama yao kuliko baba.

Baba asipokuwa na muda na familia yake ni kiashiria cha kutokujali. Pole pole baba anahamishia tabia hiyo kwa watoto wake. Kama nilivyoeleza awali, nao wakiwa watu wazima wengi wao hufanya vivyo hivyo katika ndoa zao, kwani ndicho walichojifunza kutoka kwa baba yao.

Kuhangaikia familia ni wajibu muhimu wa baba, lakini hiyo isiwe kisingizio cha kudumu cha baba kukosa muda na mwenzi wake au familia yake. Kuhangaikia mahitaji ya familia ni muhimu kuende sambamba na kutengeneza muda wa kuwa na familia ili kuleta amani na utulivu nyumbani.

**Mjenzi wa nidhamu**

Mungu amewapa akina baba misuli ya kujenga nidhamu ya familia. Kama nilivyoeleza awali, vijana wengi leo hawana nidhamu kwa sababu baba zao hawakutumia nafasi zao vizuri kuadabisha na kuelekeza wakati wakiwa watoto.

Kinababa wengi hawana muda na watoto wao. Wako mbali nao. Watoto wanapokosa malezi ya baba, kuna vitu watoto wanavikosa ambavyo ni muhimu katika makuzi bora. Ni muhimu kinababa kuzingatia jambo hili kuepuka matatizo yasiyo ya lazima hapo baadaye.

# MAISHA

JANUARI 31, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 10

## Udhaifu wa mzazi usipotoshe ukweli



## MAISHA NI NYUMBA

Usiichoke nyumba yako, ifanyie utundu uifurahie



## HARUSI

Ukurasa 12



## UNGA WA RIWA

# Hupamba ngozi laini inayong'aa

Ukurasa 14

# Udhaifu wa mzazi usipotoshe ukweli

Na Moses Ismail



NI hali inayojitokeza kwa wazazi na watoto wengi, na kila inapotokea mzazi na mtoto kila mmoja kwa wakati wake hutafuta sababu ni nini kimewafanya wawe katika hali hiyo.

Kwa vijijini, wazazi wengi hutafuta sababu za chanzo cha kutoelewana na watoto wao kupitia kwa waganga wa kienyeji. Wanachoamini wao ni lazima kutakuwa na mkono wa mtu. Iweje wao na watoto wao wasielewane?

Wanafanya hivyo pale wanapoona watoto wao wakubwa, wenye uwezo wa mali na fedha, wanashindwa kuwasaidia hata kwa mambo yao madogo tu yanayohitaji fedha. Wanaamini hilo haliwezi kutokea bila ya 'mkono wa mtu'.

Hilo limewai kutokea baina ya bibi Edith Mgaya, mkazi wa Chamazi, nje ya jijini Dar es Salaam. Yeye na mwanae hawakuwa wakielewana kabisa.

Edith anasema: "Ilifikia mahali mwanangu alikuwa hakanyagi nyumbani hata miezi minne mpaka mitano, namuona tu anapita barabarani na gari yake."

Edith akahisi si bure, lazima kuna mkono wa mtu kwa sababu mtoto wake alikuwa na uwezo mkubwa wa mali, akaenda kwa mganga. Anasimulia:

"Kumbe alikuwa amelogwa. Mganga akanipa dawa. Akaniambia nimuite na nijaribu kuongea na mwanangu kwa upole wakati natumia dawa hiyo. Leo ni mwaka wa sita sasa hatujakwaruzana."

Ni kweli, kwa imani za kiroho uchawi upo na hata vitabu vitakatifu vinaeleza madhara yake na vinakataza waumini kushiriki uchawi, lakini je, katika hili la mzazi na mtoto 'kuwa mbalimbali' ni uchawi ndio unaosababisha?

"Jibu haliwezi kuwa la moja kwa moja", anasema Denis Munga, mtaalamu wa masuala ya saikolojia na kufanfua:

"Haliwezi kuwa la moja kwa moja kwa sababu pamoja na kwamba uchawi upo na watu wanauamini, lakini katika kesi nyingi za mzazi na mtoto kutoelewana suala la saikolojia linachukua nafasi kubwa sana".

Munga anatoa mfano: "Mfano wazazi wenye tabia ya kupenda kutokaa pamoja na watoto wao, hawa wanajenga tatizo hilo wenyewe. kutopenda kuwa karibu na mtoto wako wakati akiwa mdogo kunajenga ufa baina yenu.

"Ufa huu ukiendelea kwa muda mrefu, yanakuwa ni maisha ya kawaida baina ya mzazi na mtoto, hata kama mtoto atakuwa na umri wa miaka hamsini, kwa sababu msingi ulishajengwa tangu utotoni".

Wazazi wengi wanaoshindwa kushirikiana na watoto wao katika hali ya utu uzima wanavuna matunda ya ukali waliuonyesha kwa watoto wao walipokuwa wadogo.

Hii inasaidia kwa wazazi wa kizazi hiki kujifunza jambo hilo na kurekebisha pale wazazi wao walipojikwaa kwa malezi yao.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

**Andika kitenzi Ouvrir (yaani kufungua) katika nyakati tofauti kama zilivyoainishwa hapo chini**

Indicatif
présent
j' ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous……………
vous ……………
ils/elles ……………

**imparfait**
j' ……………………
tu ……………………
il/elle ……………………
nous ……………………
vous ……………………
ils/elles ……………………

**future simple**
j' ……………………
tu ……………………
il/elle ……………………
nous ……………………
vous ……………………
ils/elles ……………………

**passé simple**
j' ……………………
tu ……………………
il/elle ……………………
nous ……………………
vous ……………………
ils/elles ……………………

**passé compose**
j' ai ……………………
tu as ……………………
il/elle a ……………………
nousavons ……………………
vousavez ……………………
ils/ellesont ……………………

**plus – que – parfait**
j' ………ouvert
tu ………ouvert
il/elle ………ouvert
nous………ouvert
vous………ouvert
ils/elles………ouvert

futurantérieur
j' ………ouvert
tu ………ouvert
il/elle ………ouvert
nous ………ouvert
vous ………ouvert
ils/elles ………ouvert

**passéantérieur**
j' eus ……………
tueus ……………
il/elleeut ……………
nouseûmes ……………
vouseûtes ……………
ils/elleseurent ……………

**Conditionnel présent**
j' ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous ……………
vous ……………
ils/elles ……………


**passé**
j' aurais ……………
tuaurais ……………
il/elleaurait ……………
nousaurions ……………
vousauriez ……………
ils/ellesauraient ……………

**Infinitif présent** ……… **passé** ……………

**Participe présent** …………… **passé** ………/….
…………/tes
ayant ……………

## WATOTO

## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

JAMAA mmoja alivamia semina ya wasomi iliyokua inafanyika maeneo ya posta, wakati wa kujitambulisha hali ilikuwa hivi.

1: Naitwa Anna niko SUA mwaka wa tatu nasomea kilimo

2. Naitwa Stella niko UDSM mwaka wa pili nasoma Uhusiano wa Umma.

3: Naitwa Emmanuel niko UDOM mwaka tatu nasomea Computer science.

4: Jamaa akainuka kisha akasema"Naitwa Elisha niko TANESCO mwaka wa saba nasoma mita".

SWALI
Ng'ombe dume anaitwaje?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Alitelekeza familia, akaishia kuuza machungwa mtaani!

NIKUKARIBISHE tena msomaji wangu katika safu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Hii ni sehemu ya pili mwendelezo makala ya wiki iliyopita, ikihusu mama mmoja aliyejitosa kulea watoto wake wanne baada ya mumewe kumteleteza.

Kwa wale ambao hawakukisoma kituko hicho wiki iliyopita ni hivi; familia ilikuwa tajiri na maisha mazuri sana. Mume akawa na tamaa ya mahusiano na wanawake nje ya ndoa.

Siku moja akaamua kumsafirisha mkewe na watoto kwenda kijijini kwa wazazi wa mke. Mume naye alienda pamoja nao ambako alikaa kwa siku mbili kisha akarejea mjini kwa kazi zake.

Mke naye baada ya mwezi akataka kurudi mjini nyumbani kwake na watoto ambao walikuwa wanahitajika kurudi shuleni. Cha ajabu, mama huyu kurudi alimkuta mwanamke mwingine nyumbani kwake.

Hakuruhusiwa kuingia ndani na hata alipompigia simu mume wake hakupatikana. Alipagawa akawa chizi wa barabarani. Hata hivyo, alipata msaada wa mlombi akapona.

Akapewa fedha za mtaji akaanza biashara ya kununua khanga na vitenge. Bibie huyu alikubali kuanza upya bila kuangalia utajiri aliowahi kuwa nao. Wakati huo watoto walikuwa kijijini hawajarudi shule bali walikuwa wakichunga mifugo ya babu yao na kulima.

Aliendelea kuuza vitenge kwa bidii na kwa sababu alikuwa tayari ameokoka, alimshirikisha Mungu kwa kila anachokianzisha.

Baada ya mwaka mmoja, yule dada alikuwa na mtaji usiopungua Sh. milioni tano kutoka Sh.50,000 alizopewa kujikimu kimaisha. Alichukua uamuzi wa kurudi Dar kuendeleza biashara ya vitenge.

Wakati huo watoto wake wakiwa tayari wamerudi shule kuendelea na masomo yao. Akafungua duka kubwa Kariakoo, akifuatia mzigo Kenya na Congo. Mungu aliendelea kumpigania, akajenga nyumba kubwa ya kifahari, watoto akawahamisha shule na kuwapeleka Nairobi, Kenya.

Mungu akaendelea kumbariki na kumfikisha hatua ya kumiliki maduka makubwa matano ya vitenge, magari makubwa ya kubeba mizigo kusafirisha mikoani. Hakika alikuwa tajiri kwa namna ya ajabu.

Baada ya miaka mingi kupita, alishangaa siku moja kumuona aliyekuwa mumewe akitembea barabarani anauza machungwa! Hakuamini macho yake kwani alihisi anaota ndoto ya mchana kutokana na kupita miaka mingi bila kuonana.

Alikuwa amemsahau. Ajabu mume wake ndiye aliyekuwa wa kwanza kumtambua kwa kumuita jina lake. Yule baba alikuwa amechoka na kudhoofu kwa namna isiyoelezeka.

Yule mama alipomuangalia, hakutaka kuendelea kumsikiliza, baba aliomba msamaha kutokana na majeraha aliyowahi kumsababishia. Lakini wakati anaondoka katika eneo lile aliona huruma ndani yake.

Huruma ile ilimsukuma amchukue na kumpeleka alipokuwa ameegesha gari lake, akampandisha na kumpeleka kwanza hospitali kwani alikuwa amedhoofu na kuonekana mgonjwa.

Baada ya vipimo kufanyika, iligundulika kuwa tayari ameathirika na virusi vya Ukimwi na vilikuwa kwenye hatua ya mwisho. Ilibidi apewe taarifa kuhusu afya yake.

Habari hizo zilimfanya aangue kilio na kumuomba msamaha aliyekuwa mkewe kwa maumivu yote aliyomsababishia. Yule mama alimsamehe, jambo ambalo katika hali ya kawaida lisingewezekana.

Yule mama aliendelea kumuuguza kwa miezi mitatu bila kumtelekeza wala kumnyanyasa. Kwa bahati mbaya alifariki kutokana na lile gonjwa.

Mpenzi msomaji, napenda nikueleze jambo moja kuwa haijalishi umetelekezwa na mume au mke unaweza kuinuka tena kama ukiamua. Haijalishi umeshushwa kiasi gani, ukimwamini Mungu na kuchukua uamuzi wa kusimama tena, utashinda tu. Mungu anasema hivi; Ayubu 22:29 "Hapo watakapokuangusha, utasema kuna kuinuka tena; Naye mnyenyekevu Mungu atamwokoa".

Yapo mazingira ambayo mtu anayatengeneza pasipo kujua kwamba ni majuto huko aendako. Atajiona ni mshindi na kwamba amemkomoa mwenzie, kumbe amejichimbia shimo mwenyewe.

Jamaa alimtelekeza mke na watoto bila kujua kuwa hiyo ndiyo familia aliyotunukiwa na Mungu. Hilo amelitambua akiwa katika hali mbaya. Pengine Mungu aliweka mazingira hayo kumuonyesha huyo baba kuwa yule ndiye alikuwa mke wa ndoto yake. Maisha Ndivyo Yalivyo.

***Mpenzi msomaji, kila tulifanyalo, tujitahidi sana kumshirikisha Mungu. Shetani amevuruga ndoa za watu wengi. Naamini yapo mengi umejifunza kupitia yaliyoisibu familia hii. Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581. Hadi wiki ijayo.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# TBS ijipange vyema ukaguzi wa magari nchini

HIVI karibuni Shirika la Viwango Tanzania (TBS), lilitangaza utaratibu mpya wa ukaguzi wa ubora wa magari yanayotoka nje ya nchi, ambao awali ulifanywa na mawakala katika nchi za Dubai na Japan.

Kwa sasa gari baada ya kuwasili nchini litakaguliwa ubora wake na TBS na kama litakuwa na marekebisho yoyote yatafanywa katika gereji maalum zilizotambuliwa na shirika hilo. Wakati huo huo mteja atawajibika kugharimia matengenezo kama gari lake litakuwa na ubovu wowote.

Serikali inasema uamuzi huo umefikiwa ili kuongeza mapato tofauti na awali ambapo ukaguzi ulifanyika katika nchi ambayo chombo cha usafiri kinatoka na kupewa cheti cha ubora ambacho kilikuwa lazima kikaguliwe bandarini mara baada ya chombo kufika.

TBS imesema gharama za huduma hiyo ni Sh. 300,000 na awali ilikuwa Dola za Marekani 150 kwa gari moja na kampuni aliyotumia mtu kuagiza gari ndiyo ilisimamia ukaguzi na kupata cheti cha ubora.

Tangu kufikiwa uamuzi huo kumekuwa na maswali mengi ambayo ni muhimu sana yakajibiwa, kwamba kwa sasa usalama wa vyombo wanavyoagiza Japana na kwingine utakuwaje kwa kuwa waliokuwa wanawauzia magari walijua kuna ukaguzi wa ubora unafanyika nchini humo, wakalazimika kuhakikisha chombo husika kipo katika hali nzuri.

Kwa kawaida mtu anapotaka kununua gari anaingia kwenye mtandao wa mawakala wanaotambulika duniani wenye ofisi katika nchi gari linakotoka na linakokwenda ambao huonyesha picha mbalimbali za gari husika ambazo ni rahisi sana kumdanganya mtu kuwa chombo hicho ni bora.

Ukishajiridhisha na chombo husika kwa kuona picha basi utatakiwa kufanya malipo kwa njia ya benki ndipo utaratibu wa kusafirisha chombo hicho unaanza, na kwa utaratibu wa sasa ukaguzi utafanyika nchini na ndipo mteja atajua kama chombo chake ni bora au la.

Lingine ni matengenezo na uwezo wa kuhifadhi magari yaliyo kwenye matengenezo, kwamba sasa gharama zitaamualiwa na wanaotengeneza na kadri wanavyokuhifadhia chombo hicho katika karakana yao maana yake utawajibika kufanya malipo flani fulani.

Ni muhimu sana kwa utaratibu huu mpya wananchi wakatolewa hofu kwa kuhakikishiwa kuwa anapoagiza chombo husika kwa kujiridhisha kutoka kwa mawakala husika basi anapata chombo salama kulingana na thamani ya fedha aliyotoa, kwa kuwa hatakuwa na uwezo wa kwenda Japan au Dubai kufuatilia zaidi.

Kwa utaratibu huu, hofu ni kuwa huenda wananchi wakapoteza fedha nyingi kwa ajili ya kugharamia matengenezo au kwa kuambiwa kuwa chombo chake hakina ubora wa kutumika nchini. Maana yake fedha iliyotumika kuagiza imepotea na sasa kuna gharama za ukaguzi na matengenezo.

Ni muhimu sana kukawa na ufuatiliaji wa mawakala wanaouza magari kwenye nchi hizo na wana matawi yao nchini, ili kuepusha wananchi kuuziwa vyombo vya usafiri chakavu na kushindwa kudai fedha zao.

Ukaguzi kufanyika nchini ni manufaa kwa serikali kwa kuwa sasa mapato yataingia serikalini tofauti na awali fedha hizo zilikwenda kwa mawakala hao, lakini utaratibu huu mpya ni muhimu usimamiwe vizuri ili kuhakikisha hakuna maumivu kwa wananchi.

Ni muhimu sana karakana zitakazohusika na ukaguzi wa magari zikawa na watu weledi wa kazi hiyo, kulinda na kuzuia mianya yote ya rushwa ambayo kwa kiasi kikubwa itaongeza gharama na maumivu kwa wananchi.

Iko changamoto kubwa ya utendaji kazi wa baadhi ya wafanyakazi wa taasisi, mashirika na serikalini kwa kuwa hakuna usimamizi wa karibu kama ilivyo sekta binafsi, na wengi wamejikuta katika utendaji kazi wa kimazoea ambao kwa kiasi kikubwa ni maumivu kwa wanaosubiri huduma.

Waziri wa Viwanda na Biashara alieleza kuwa watachukuliwa vijana kutoka chuo cha Usafirishaji Tanzania (NIT) na Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT), ambao watapata mafunzo maalum kutoka kwa wataalam kutoka nje, ili waweze kufanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Pamoja na kuandaa vijana hao ni muhimu kuwa na vifaa vya kisasa vya ukaguzi ili kazi hiyo ifanyike kwa ufanisi na kwa wakati, kuliko kuingia kwenye ucheleweshaji ambao moja kwa moja utazalisha urasimu na rushwa kwa wananchi.

***Tutafakari!***

# HARUSI









Ilikuwa furaha na nderemo kwa ndugu na jamaa wa Michael Mlanda na Sara Michael baada ya kufunga ndoa hivi karibuni mkoani Tanga.



# MITINDO



## KIZIBAO

## Vazi linalopamba joto

KIPINDI hiki cha joto, watu wanapata shida kupata mavazi ambayo yatawatoa maridadi bila kusumbuliwa na hali ya hewa ya uvuguvugu.

Mavazi mazito kama suti na koti katika kipindi hiki inakuwa vigumu kuvaliwa, watu wengi wanatumia njia mbadala ambazo wanaweza kuonekana tofauti.

Hata hivyo, kizibao ni moja ya vazi linalofaa katika mazingira ya joto kutokana na kuruhusu hewa kupita kwa urahisi.

Pale mtu akivaa kizibao anaonekana nadhivu, mtanashati na mwenye mvuto wa kipekee.

Hata hivyo wanaume wengi hawafahamu njia nzuri ya kuvaa vazi hili, kitu ambacho inapelekea wengi wao kuvaa tofauti..

**UREFU**

Kizibao kinatakiwa kiishie juu ya mkanda wa suruali, hakikisha kisiwe kifupi sana kwa sababu inatakiwa kuziba sehemu ya muonekano wa shati.

**MWONEKANO**

Hakikisha mwonekano wa kizibao unakuwa mzuri na wenye kuvutia. Kama kizibao kimewekwa mkanda hakikisha unafunga kwa alama ya X ili kukupa mvuto zaidi.

Shati safi

Unashauriwa shati unalovalia kizibao lazima liwe safi na lenye mtindo wa kisasa.

**RANGI**


Jambo muhimu ni kulinganisha rangi ya kizibao na shati la ndani, kama kizibao kina rangi ya dongo au nyeusi, hakikisha shati linakuwa na rangi nyeupe au rangi yenye kung'aa.

Wataalamu wa mitindo wanasema kabla ya mtu kuamua kuvaa kizibao, lazima ufanye chaguo sahihi la rangi.

## UREMBO







UNGA WA RIWA

# Hupamba ngozi laini inayong'aa

MWANAMKE anakuwa na furaha zaidi pale anaposifiwa kuwa ana sura ya kung'aa, ngozi laini na hana makovu mwilini.

Hata hivyo, baadhi ya wanawake wanajiuliza wafanye nini ili kuwa na sifa hizo.

Wataalamu wa urembo wanasema sifa hizo zinaweza kutoweka kama mwanamke ataathiriwa na chunusi wakati wa ukuaji na hata akiwa mkubwa.

Wanasema chunusi inapokaa kwa kipindi kirefu bila kupata ufumbuzi, husababisha uso kutawaliwa na makovu kutokana na kutumbuliwa bila kufuata utaratibu.

Kwa ujumla chanzo cha chunusi inatokana na mabadiliko ya mwili wakati wa kuingia katika ujana au ngozi zenye mafuta.

Lakini wapo wanaopata matatizo haya kutokana na matumizi ya vipodozi bila kuzingatia ushauri wa kitaalamu.

Hata hvyo kuna njia rahisi za kuondoa makovu yanayotokana na chunusi.

**MAHITAJI**

Unga wa riwa, maji ya waridi (Rose water),maji safi ya kawaida, limao na mafuta ya mzaituni.

**HATUA YA KWANZA**

Chukua unga wa riwa na maji ya waridi,changanya vizuri hadi mchanganyiko uwe mzito.

**HATUA YA PILI**

Upake mchanganyiko wako katika sehemu yenye makovu, kisha acha hadi ukauke. Unaweza kukaa na mchanganyiko kwa muda wa nusu saa ili kusaidia kunyonya mafuta na kuacha ngozi kuwa kavu.

Ukiona imekauka, nawa vizuri na maji ya uvuguvugu.

**HATUA YA TATU**

Paka Juice ya Limao kwenye sehemu yenye makovu, hapa inatumika kama tiba ya asili ambayo husaidia kufifisha madoa.

**HATUA YA TANO**

Paka mafuta ya mzaituni kwenye makovu, hii husaidia kulainisha ngozi na kutoa makovu.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Utamu wa kashata na kahawa

KASHATA ni moja ya vyakula ambavyo watu wengi wanapenda kula, lakini hawajui namna ya kutengeneza wakiwa nyumbani.

Wengi wanadhani zinatumia muda mrefu kutengeneza na ndio sababu wanaogopa kuziandaa.

Pia wapo ambao hawapendelei kula kwa sababu ya kuhofia mazingira ya uandaaji wake, hivyo ni wakati mwafaka sasa wa kuanza kula.

Badala ya kununua kashata mitaani unaweza kuungana nami kujifunza namna ya kutengeneza na wewe ukafanya hivyo ili kufurahia na familia yako.

Kuna aina mbalimbali za mapishi ya kashata lakini leo tutaelekezana namna ya kupika kashata za karanga.





**MAHITAJI**

Karanga kilo moja, sukari vikombe vitano, maji vikombe viwili, maziwa ya unga vijiko vya chai vya chai viwili.

**Namna ya kutayarisha na kupika:**

Kaanga karanga zako kawaida baada ya kuzisafisha na kuhakikisha hakuna iliyooza.

Saga karanga zako vizuri hadi zilainike kwa kutumia kinu au chupa na kibao cha kusukumia chapati.

Kisha changanya maji na sukari weka jikoni yachemke mpaka yanate kidogo kama shira.

Changanya unga wa karanga na maziwa ya unga, kisha mimina kwenye shira.

Koroga taratibu kwa moto mdogo mpaka uone imeshikana na inanata.

Paka mafuta kwenye sahani kisha mimina na utandaze.

Acha ipoe kidogo, halafu katakata vipande na acha ipoe kabisa.

Panga kwenye sahani tayari kwa kuliwa pamoja na kahawa.

## MAISHA NI NYUMBA

# Usiichoke nyumba yako, ifanyie utundu uifurahie

**Na Elizabeth Zaya**

BAADA ya miaka kadhaa ya kuishi kwenye nyumba, wengi hutamani kubadilisha mwonekano wake.

Pia mara nyingi wamiliki wengi wa nyumba hupendelea kurekebisha jengo au kununua samani mpya ambazo hutumia gharama kubwa.

Andiko hili la leo ni kukupa mwanga tu namna ya kuboresha maisha ya nyumbani kwako kwa gharama nafuu na ukabaki unafurahia maisha.

Kubadili rangi ya nyumba yako, mapambo au karatasi za ukutani, vitambaa na malighafi nyingine zilizotengenezea samani zako vina nafasi kubwa ya kubadilisha kabisa muonekano wa nyumba yako na kukupa wa kuvutia zaidi.

Pia kupaka rangi upya kabati la luninga au meza, kubadili kitambaa kilichotengenezea viti au sofa, nako kunasaidia kubadilisha mwonekano katika nyumba yako.

Nyingine ni kubadili vitu vinavyoonekana ni vidogo kama vile tai na fimbo za pazia, pazia zenyewe na zuria, vinachangia kwa kiwango kikubwa kuleta mwonekano mpya na mzuri kwenye nyumba.

Viko vitu vingi ambavyo unaweza kuvifanyia marekebisho kwa gharama ndogo ndani ya nyumba yako na ukaifurahia tena na usiichoke, kwa mfano kujiwekea utaratibu wa kubadili rangi ya ukuta mara kwa mara unapoona unaiochoka ya awali.

Pia hata kuchagua kubadili kitu kingine unachoona unatakiwa kufanya hivyo. Kama ni foronya unatakiwa kuangalia zile zinazoendana na zilizoko kwa wakati wa sasa.

Kama vitu vyako vya ndani umevitumia kwa miaka mingi na vimepitwa na wakati na vinachangia uione nyumba yako inakuchosha na hata kuiona mbaya, usikate tamaa, tumia njia hiyo kwa kufanyia marekebisho kitu kimoja baada ya kingine na utaanza kuifurahia tena.

Kikubwa ni kuwa mbunifu na kuongeza taratibu vionjo vinavyoendana na wakati katika nyumba yako. Hata kama huna kipato kikubwa inawezekana, si lazima uweke vyote kwa pamoja, kadri unavyojaaliwa unabadili cha zamani na unaweka kinachoendana na wakati.

Utanunua pazia leo lakini siku nyingine kitu kingine na hii pia itasaidia nyumba yako kuonekana mpya kila siku.

Ni ukweli kuwa vitu vya nyumbani vinabadilika kila baada ya kipindi kifupi, zuria ulilonunua miaka mitano iliyopita, haliwezi kuendana na wakati huu.





## MPANGILIO

# Dondoo muhimu ya namna ya kupamba nyumba kwa matunda

**1:** Katika kipindi cha mavuno mapambo yanayotokana na vyakula asili yanaweza kukupa furaha. Hakikisha mlangoni unaweka maua ambayo yanaonyesha matunda.


**2:** Sebuleni unaweza kuweka kupambo tofauti ya vyakula kama maboga, machunga, limao na tawi la mti katika meza.

**3:** Chumbani unatakiwa kuweka meza maalum ambayo aina mbalimbali ya vyakula vitaonekana kwa urahisi. Weka maboga, mahindi, maua asilia na tawi la mchungwa wenye matunda.

**4:** Chumba cha chakula weka mapambo ya vyakula vyenye kuongeza hamu, kama limao, nanasi, chungwa, tikiti maji na maboga. Weka katika mpangilio wa kuvutia.



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
PAPARA ZAKO ZIMEHARIBU KILA KITU! UNGESUBIRI
UMBEA HAUNA SUBIRA
VIJORA, KANGA VITENGE, CHENI HERENI, VIKUKU LENDI'KRUZA USHAWAIGI KUPEWAGA?
ACHA MBWEMBWE SEMA UNA'SHING NGAPI?
UNAJUA UMEPOTEA!
MBONA SIJAULIZA NJIA?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
JUKWAANI
ZILE AHADI ZAKO MIMI NILIJUA TU, 'HUTOBOI' ILA NILIKUWA NAKU-ANGALIA...
KWA HIYO ULIKUWA UNA-SUBIRI MGONJWA AFE, NDO USEME ULIJUA DAWA
AFANDE! UNAANDIKA FAINI HUANGALII HATA 'PESONALITI' YA MTU!
NDIO MAANA NAKUANDIKIA 'TISINI' NIME-ZINGATIA HILO
TOFAUTI NA ZAMANI, SIKU HIZI UKIRUDI KAZINI UNAKUWA NA MAWAZO RUNDO!
NISIWAZE MCHEZO!
...DOMO LA MBEA HALIFUMBI...

# HABARI KIMATAIFA



Ofisa wa Umoja wa Mataifa akiangalia majengo yaliyobomolewa katika ghasia zinazoendelea kati ya waasi na vikosi vya serikali ya Jamhuri ya Afrika ya Kati, hivi karibuni **(PICHA: DW)**

## Waziri mkuu DRC ajiuzulu

**KINSHANSA, DRC**

WAZIRI Mkuu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Sylvestre Ilunga Ilunkamba, amejiuzulu nafasi yake baada ya jana kuwasilisha barua yake kwa Rais Félix Tshisekedi.

Ilunga, ambaye ni mshirika mkuu wa Rais mstaafu wa nchi hiyo, Joseph Kabila, aliongoza baraza la mawaziri la serikali ya Muungano kwa miezi 15.

Hatua hiyo imekuja baada ya wabunge kupiga kura ya kutokuwa na imani na serikali yake siku ya Jumatano ya wiki hii na kupewa saa 24 awe amejiuzulu.

Kujiuzulu kwake kunatoa fursa kwa Rais Tshisekedi kuwateua mawaziri ambao watatoka katika kambi ya washirika wake.

Utendaji wa Rais Tshisekedi umekuwa ukidhibitiwa na wabunge wa muungano wa vyama vinavyomuunga mkono Kabila.

Rais Tshisekedi bado hajamchagua waziri mkuu mpya, ambaye atataunda serikali mpya. **BBC**

## Uganda yaongoza kwa rushwa Afrika Mashariki

**KAMPALA, Uganda**

UGANDA imetajwa kuongoza kwa vitendo vya rushwa kwa nchi za Afrika Mashariki.

Kulingana na ripoti mpya ya shirika la kimataifa la Transparency ya mwaka 2020 iliyohusisha mataifa 180, Uganda imeshika nafasi ya 142.

Ripoti hiyo iliyoangazia ufisadi kwenye janga la Covid 19, inaonyesha nchi za Tanzania, Kenya na Rwanda zimefanya vizuri katika kudhibiti rushwa na ufisadi katika sekta hiyo ya afya.

Nafasi hiyo ni tofauti ya mwaka 2019, ambapo ilishika nafasi ya 137 kati ya mataifa 180.

Mkurugenzi wa shirika la Transaprency International nchiniUganda, Peter Wandera, alisema Ripoti hiyo ni ya kimataifa ya masuala ya ufisadi inayotolewa na mataifa mbalimbali duniani kwa wakati mmoja kulingana na viwango vya ufisadi.

**Licha ya Uganda kuonesha jitihada katika mapambano ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona, kuna tuhuma za ufisadi zinazotokana na kushindwa kuonesha matumizi halisi ya rasilimal**

"Mwaka 2020 janga la corona limesababisha ufisadi zaidi, katika ripoti hiyo inaonesha kwamba, mataifa mengi yaliyotajwa kupanda kwa vitendo vya rushwa imetokana na kushindwa kusimamia rasilimali za kupambana na Covid-19." Alisema Wandera.

Aliongeza "Licha ya Uganda kuonesha jitihada katika mapambano ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona, kuna tuhuma za ufisadi zinazotokana na kushindwa kuonesha matumizi halisi ya rasilimali."

Ripoti hiyo inaonyesha mwaka 2020, robo tatu ya mataifa yaliyoshiriki yalipata alama chini ya 50

Hii inamaanisha kuwa rushwa ipo si katika sekta ya afya pekee, bali hata katika demokrasia.

Mataifa mengine ya Afrika Mashariki yaliyofanya vizuri ni Rwanda ikishika nafasi ya 49, Tanzania 94, Kenya nafasi ya 124.

Hata hivyo, serikali ya Uganda hazijatoa tamko lolote kuhusu ripoti hiyo.

**BBC**

## Mtoto ahifadhi mwili wa mama yake ndani ya jokofu

**TOKYO, Japan**

POLISI wa Japan wamemkamata mwanamke mmoja akituhumiwa kuuficha mwili wa mama yake ndani ya jokofu kwa muda wa miaka 10.

Mwili huo ulikutwa umewekwa ndani ya jokofu nyumbani kwake katika mji wa Tokyo.

Yumi Yoshino (48) alijitetea kuwa alimkuta mama yake akiwa amefariki kisha aliuficha mwili wake kwa miaka yote hiyo kwa sababu hakutaka kuhama katika nyumba waliyokuwa wakiishi.

Vyombo vya habari viliwanukuu maofisa wa polisi ambao hawakutajwa majina yao kuwa mwili wa mwanamke huyo haukuonekana na majeraha yoyote licha ya kugandishwa kwenye barafu.

Hata hivyo, hawakuweza kuthibitisha muda na sababu ya kifo cha mwanamke huyo.

**BBC.**

## Viongozi Maziwa Makuu wataka amani CAR

**LUANDA, Angola**

VIONGOZI wa Afrika kutoka eneo la maziwa makuu wamewatolea mwito waasi wa Jamhuri ya Afrika ya Kati kukubali kusitisha mapigano.

Waziri wa mambo ya nchi za nje wa Angola, Tete Antonio, alisema viongozi hao wamekubaliana kuwa wanataka eneo la maziwa makuu lisilokuwa na vurugu, vifo au watu kukosa makazi.

Mkutano huo uliofanyika mji mkuu wa Angola Luanda, na kuhudhuriwa na Marais wa Congo Brazzaville Denis Sassou-Nguesso na Paul Kagame wa Rwanda.

Viongozi hao walikubaliana kuunga mkono ombi la nchi hiyo lililotolewa kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa la kuondolewa vikwazo vya silaha nzito ambazo inazihitaji kupambana na waasi hao.

Waasi hao wanaodhibiti theluthi mbili ya taifa hilo, walianzisha mashambulizi wiki moja kabla ya uchaguzi mkuu uliomrejesha madarakani Rais Faustin Archange Tou-adera.

Umoja wa Mataifa ulisema ghasia za uchaguzi nchini humo zimesababisha watu zaidi ya 200,000 kukosa makazi.

**DW**

## Katiba mpya Syria yakwama

**GENEVA, Uswisi**

MAZUNGUMZO juu ya kuunda katiba mpya ya Syria yaliyouhusisha serikali na wapinzani yamegonga mwamba.

Mpatanishi wa Umoja wa Mataifa Geir Pedersen, alikiri hakuna kilichofikiwa katika mazungumzo hayo yaliyofanyika mjini Geneva nchini Uswisi kwa muda wa wiki moja.

Pedersen, alisema mapendekezo yaliyotolewa na wapinzani juu ya kusogeza mbele mazungumzo yalikataliwa na wajumbe wa serikali.

Mwaka uliopita kamati maalumu ya katiba ya Syria iliundwa kwa lengo la kuutatua mgogoro wa nchi hiyo ili kumaliza vita vya wenyewe kwa wenyewe.

**DW.**

SAFU

# Siku ya kifo changu ni nani atakayenililia?



Na Magabilo Masambu

UKOMO wa maisha ya mwanadamu umeelezwa katika vitabu mbalimbali vya dini na vya kidunia (sayansi) kwamba mwanadamu atazaliwa lakini siku moja atakufa na kutoweka duniani.

Lakini baadhi vitabu vya dini vinaeleza juu ya uwapo wa maisha mengine baada ya kifo. Hii ina maana kwamba hakuna mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke atakayeishi milele.

Kila mmoja wetu yuko duniani kwa kusudi maalumu pamoja na kwamba inawezekana ukazaliwa, ukaishi na ukaondoka bila kufahamu kusudi la kuwapo duniani. Hivyo kila mmoja wetu aliye hai anayo kazi ya kutafuta kusudi la kuwapo duniani.

Wakati tunaendelea kuishi ni muhimu sana kila mmoja wetu kujiuliza "Siku ya kifo changu ni nani atakayenililia? Maisha yana maana tuwapo hai lakini yana maana zaidi kama tutayagusa maisha ya watu wengine. Duniani tumeumbwa ili tutegemeane, pengine tungekuwa kila mmoja wetu amejitosheleza kwa kila kitu, inawezekana maisha yangekosa maana.

Pamoja na kuhangaika juu ya maisha yetu binafsi, ni muhimu sana kujiongezea idadi ya watu watakaokulilia kwa dhati siku ya kifo chako. Hii ina maana gani hasa? Kila mmoja wetu akiwa na fikra hizo basi upendo miongoni mwetu utaongezeka maradufu na maisha yatakuwa na maana zaidi.

Tunahangaika sana juu ya kujenga vitu duniani. Si jambo baya lakini ni rahisi sana kumbukumbu kubakia kwa watu uliyogusa maisha yao, kuliko majengo na mali nyingi utakazokuwa umeziacha.

Wakati mwingine mali utakazoziacha zinaweza kuwa vyanzo vya migogoro mikubwa. Simaanishi tusiwekeze lakini tukiwekeza katika maisha ya watu, utakuwa uwekezaji utakaoacha alama kama wasemavyo siku hizi.

Unaweza kuwa na madaraka, mali, fedha na vitu vinginevyo vya namna hiyo lakini vyote hivyo ni vya kupita. Ukifanikiwa kuwa navyo basi uvitumie kuleta furaha kwa watu wengine ambao kwa hakika hata siku haupo watabaki kukumbuka kwamba ulikuwapo.

Mark Cahill katika kitabu chake kinachoitwa "One Heartbeat Away" anauliza When you die, what do you think will be on the other side? Akimaanisha wakati utakapokufa, unafikiri ni nini kitakuwa upande wa pili? Kwa maana ya maisha baada ya kifo.

"Msistaajabie maneno hayo, kwa maana saa yaja, ambayo watu wote waliyomo makaburini wataisikia sauti yake, nao watatoka.Wale waliyofanya mema kwa ufufuo wa uzima na wale wliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu (Yohana 5:28-29). Unaposhindwa kutengeneza watu watakaokulilia kwa kutokuwepo kwako maana yake, kuna uwezekano mkubwa unatengeneza watu watakaofurahia na kusherekea siku haupo. Tafasiri yake unawatendea mabaya watu hao.

Natambua kwamba si kila utakayemtendea mazuri atakushukuru na kuona umuhimu wako, lakini miongoni mwa wabaya hawakosekani wema, ambao watasema bila fulani nisingefika hapa nakadhalika.Lakini hatupaswi kukata tamaa kwa sababu kuna muda unaweza kuwasaidia watu wakati ambao hawana uhitaji bali siku uhitaji huo utakapowapata, watakumbuka na misaada ya nyuma, hapo ndipo watakapokulilia wakati haupo.

Wakati mwingine hata baadhi ya unaowasaidia wanaweza kugeuka na kuwa adui zako, wanakusema vibaya kwa watu, wanakufitini hii ni kwasababu ni vigumu sana kutambua mchango wa mtu akiwapo, bali atakapoondoka ndipo pengo lake litakapoonekana. Pengo hilo maranyingi ndilo linalowafanya watu walie sana siku ya msiba na pengine maisha yao yote.

Adui wa binadamu si wanyama wa mwituni tu bali ni binadamu mwenyewe. Dunia hii itakuwa salama tu pale kila mmoja wetu atakapotenda wema kwa mwenzake. Ubaya wa wengine husababishwa na ubaya wetu pia kwa sababu kama binadamu anaweza kujifunza wema anaweza kujifunza ubaya pia. Kama huna uwezo wa kuwasaidia basi angalau usiwaumize.

Pengine nisieleweke kwamba wenye uwezo wa kusaidia wengine ni wale wenye mali nyingi, au madaraka makubwa hapana vitu unavyoviona kwamba ni vidogo kwako, ndivyo vinavyogusa maisha ya wengi. Kuna mtu anaweza kukosa Sh. 100 ili iwe 400 apande daladala, unaweza kuona ni kitu kidogo sana lakini hiyo Sh. 100 itamfikisha nyumbani na atakushukuru sana maishani.

Mwisho ni bora kuwa na watu wengi watakao kulilia na kukushukuru maishani kuliko mali na madaraka yasioishi.

***0689157789***
***magabilomjalifu@gmail.com***
***ARUSHA-TANZANIA***

# Kombolela, mchezo uliofundisha watoto 'intelijensia'



Na Adam Fungamwango

KUMEKUWA na mijadala mbalimbali kwa wazazi wa zamani na wa sasa jinsi ya malezi ya watoto. Wa zamani wamekuwa wakiwalaumu wazazi wa sasa kuwa wanawalea kwa kuwadekeza kiasi kwamba wanapata shida kwenye maisha yao ya baadaye.

Wanadai kuwa wimbi la vijana kutokuwa wabunifu, kukosekana kwa vipaji vingi kama ilivyokuwa zamani, hata vijana wengi kutegemea kuajiriwa zaidi badala ya kujiajiri na kutumia fursa zilizopo ni matokeo ya malezi ya kisasa ambayo watoto wanalelewa 'mikononi' zaidi na kufanyiwa kila kitu na wafanyakazi wa ndani.

Ukiangalia sana unakutana na ukweli kuwa watoto wa miaka ya karibuni wamekuwa hawapewi uhuru wa kuchangamana na watoto wenzao ili kila mmoja kujifunza kutoka kwa mwenzake. Badala yake wanakutana shuleni tu. Wakitoka hapo kila mmoja anakuwa nyumbani kwake, wakicheza ndani, kila mmoja geti likiwa limefungwa.

Wazazi wa kisasa wanajitetea kuwa inatokana zaidi na sababu ya kimazingira. Zamani mazingira yalikuwa yanaruhusu hali hiyo, tofauti na sasa.

Inawezekana wazazi wa pande zote mbili wakawa na hoja. Lakini ukweli unabaki pale pale kuwa watoto wa zamani walikuwa wanajikusanya mitaani na kuwa na michezo mingi ya kitoto ambayo kwa kiasi kikubwa iliwafanya wawe na furaha muda wote, hata kama nyumbani kwao kulikuwa na shida na dhiki.

Michezo hiyo iliwafanya watoto wawe wa uwezo wa kufikiri sawa sawa, afya bora na uwezo wa kuchanganua mambo na mengine ambayo yanakuja kuwasaidia ukubwani kwenye mausuala ya maisha ya kawaida tu.

Kila mchezo, pamoja na kuburudisha ulikuwa na mafunzo na lengo lake. Baadhi ya michezo ilikuwa na lengo la kuwafundisha watoto 'itelejensia'. Ni uwezo wa kujifunza kufikiri na kuelewa mambo kwa njia ya kutumia akili ya ziada.

Iletejensia kwa kawaida ni neno pana sana ambalo linaanzia kwenye ukusanyaji wa taarifa kwa njia ya siri kwa kazi za majeshi na serikali zote dunani, lakini kuna hii ya maisha ya kawaida tu.

Hata kwenye maisha ya wakaida tu binadamu anatakiwa awe na itelejensia, ingawa si wote wako hivyo.

Iko mingi, lakini leo nitasema michache tu kama 'kula mbakishie baba'. Huu ni mchezo ambao watoto wa zamani wanakusanya lundo la mchanga na kuweka mti au kijiti kati. Watauzunguka mchanga huyo na kuanza kuimba 'kula mbakishie baba', kila mmoja akipunguza mchanga kwa mkono kwenye mkusanyiko ule wa mwisho watakayoupunguza na kijiti kuanguka, basi atapigwa hadi pale atakapokwenda kushika kitu chochote ambacho kimewekwa na kukubaliwa na wote wanaocheza mchezo huo kuwa anayeshika hicho hapigwi tena. Kitu hicho kinakuwa ni mti, nyuma, mlango, au chochote kile ambacho kipo mita kadhaa kutoka hapo.

Ulionekana kama ni mchezo wa hatari, lakini uliwafundisha vijana kuwa makini, wepesi, wajanja, na uwezo wa kukabiliana na hatari iliyoko mbele yao kwa haraka.

Fikiria mtu anaangusha kijiti, anainuka haraka, afanye kazi ya kuwapiga chenga wenzake na kukimbilia kule ambako anatakiwa aende akashike ili asipigwe. Wakati mwingine mtoto anafika huko keshapigwa vibao kadhaa. Na kuna watoto wengine huwa wanazuia njia, lakini unatakiwa upambane ili ufike.

Kombolela ni mchezo mwingine ambao wengine wanakwenda kujificha, mmoja anakuwa analinda chupa moja ya plastiki ikipigwe teke na yoyote aliyekuwa amejificha.

Kanuni ni kwamba wa kwanza kutajwa ndiye anayelinda au kusafa kama lugha ya mchezo inavyosema.

Msakaji atamtaja mmoja mmoja atayejitokeza kwa lengo la kutaka kubutua au kupiga teke chupa ile kabla hajaifukia. Chupa ikipigwa teke kabla hajataja jina, basi wote waliotajwa watarudi tena kujificha na yeye ataendele, hadi atakapofanikiwa kutaja wote. Hii inamfanya msafaji awe makini mno.

Inawafanya hata waliojificha wafanye mbinu za ziada ili kufikia chupa na kuibutua. Iliwafanya watoto kuwa wabunifu mno. Inafikka wakati wanabadilishana hadi mashati ili kumchanganya msafaji.

Asipokuwa makini atasema 'kombolela Abdallah', halafi chupa ikibutuliwa, anashtuka kuona hakuwa Abdallah, ila ni Joseph. Na wale ambao wameshatajwa majina kabla ya kubutuliwa wanarejea tena kujificha na msakaji anaanza upya.

Ilikuwa burudani sana kucheza au kuangalia michezo hiyo. Hii iliwafundisha watoto 'itelejensia', ikiwa na maana ya kuwa makini, uelewa na akili ya ziada ya kung'amua vitu mbalimbali, au hatari inayokuja mbele yake kabla hata haijatokea. Wakati mwingine tu kuhisi kitu kisicho cha kawaida. Au kutoamini kila kinachosema au kufanywa bila ya kuwa na uhakika na ushahidi wa kutosha.

Kuna michezo mingine kama 'kioo'. Ni mchezo ambao watoto wawili wanashikana mikono kwa juu, na kuruhusu wengine kupita chini ya mikono hiyo, lakini mwisho wa wimbo huo wanapimba 'wa mwisho akamatwe atiwe gerezani', wanarudisha mikono chini na kumbana mmoja ambaye wimbo unapoisha na yeye ndiye yupo hapo kati.

Mchezo huu nao ulikuwa unawafundisha watoto kuwa makini na kila wanachofanya. Na pia kuchukua tahadhari wanapohisi sehemu yenye hatari.

Ndiyo maana wakati unaanza kuimbwa, wanapita kwa mwendo wa kawaida, katikati ya wimbo, wanapita haraha haraka, lakini karibia wimbo unapotaka kumalizika, wanakuwa makini mno, wanapitia kila mmoja, akitaka usiishe yeye akiwa katikati.

Mbali na kioo, michezo mingine ni 'yai bovu', 'ukuti ukuti', 'marede', 'kipande' na mingine mingi ambayo watoto wa zamani waliicheza na kuwa burudani tosha kwao na hata kwa wanaokuwa wakiwatazama.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risasi ziliwafanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu.
Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya Toyota IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini aliyemteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji?
Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu-7

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Neema aliangua kilio. Kilio kilichofuatia kumkumbatia kwa nguvu Jerry. "Jerry nisaidie Jerry, sasa tutafanyaje ili mimi nimpate mtoto wangu Diana..."

Kwa mbali Jerry alihisi msisimko wa faraja. Kukumbatiwa na mwanamke anayempenda ilikuwa ni jambo la furaha sana. Lakini kwa wakati huo mwanamke hakuwa na furaha. Hivyo naye hakutaka kuusikilizia sana msisimko alioupata.

"Usilie mama. Ndiyo maana nimekuita hapa ili tujue nini tunafanya mimi na wewe ili kumwokoa mtoto kwenye mikono ya mtekaji sawa?"

"Kumbe kweli Jerry nimeamini unanipenda. Yaani umeamua kumfutilia mtekaji hadi akoishia kwa ajili yangu?" Aliongea Neema kwa sauti ndogo, akiwa hajui kama anamwuliza Jerry au anamjibu.

"Hilo halina maana kwa sasa. Kikubwa hapa ni kutafuta mbinu za kumpata Diana wako." Alisema na kunyamaza huku bado akiwa ameegemewa na Neema.

"Kwa sasa ninachoomba siri hii iwe kwetu sisi wawili tu kuwa mtoto alipelekwa wapi. Mumeo asijue na wala kwa sasa tusiripoti polisi kwa sababu chochote tutakachofanya haraka haraka tunakosa mwana na maji ya moto. Hatujui mtoto huko yuko kwenye hali gani. Tunachotakiwa tujue kwanza mtoto bado yumo mle ndani? Yuko hai? Yuko na nani?

"Nadhani baada ya hapo huko mbele tutajua cha kufanya sawa?"

"Mimi nakusikiliza wewe tu. Nitafuatisha vile utakavyoniambia. Mradi tu mtoto wangu apatikane."

**********************************

"Unajua Neema mimi sitaki upuuzi."

"Upuuzi wa nini baba Diana, mbona hunionei huruma wewe?"

"Mimi ndiyo unionee huruma, hapa kuna kitu kimejificha ambacho mimi sikielewi."

"Huelewi nini. Huelewi mtoto ametekwa au?"

"Hapana. Ninavyojua mtoto si pesa. Watekaji wa kawaida wote wanapomteka mtu au mtoto lengo lao linakuwa pesa. Mbona hawa wiki nzima sasa na siku tatu hizi, inalekea kwenda wiki ya pili, hakuna hata dalili ya kupiga simu kusema wamemteka wanataka pesa ili wamwachie mtoto?"

Benson alimpasha mkewe na kumzodoa pia. Ni maneno ambayo aliyapata kutoka kwa ndugu zake. Kaka zake, wadogo na dada zake.

**Kwenye kikao chao kilichofanyika jana yake Gongolamboto nyumbani kwa marehemu baba yao, juu ya kutekwa mtoto, ndugu wengi walionyesha wasiwasi juu ya aina hiyo ya utekaji.**



Kwenye kikao chao kilichofanyika jana yake Gongolamboto nyumbani kwa marehemu baba yao, juu ya kutekwa mtoto, ndugu wengi walionyesha wasiwasi juu ya aina hiyo ya utekaji.

Mara nyingi watekaji hufanya hivyo kwa sababu ya kutaka pesa. Kwa maana hiyo ilitegemewa siku ya pili tu tayari mtekaji au watekaji wawe amempigia simu mke, mume au mtu yoyote mwenye nasaba naye kutaka kile wanachohitaji ili wamuachie wanaomshikilia. Au kueleza ni kwa nini wamefanya vile.

Kitendo cha kuwa kimya, kiliwafanya ndugu kuhisi kuna jambo. Na jambo lenyewe liko kwa mke.

Walikuwa na wasiwasi kuwa huenda mke wa ndugu yao alikuwa na uhusiano na mwanamume mwingine wakati akiwa kwenda ndoa na ndugu yao, hivyo huenda mtekaji nia yake ilikuwa ni mtoto na si nyinginevyo.

Maneno ya Ben yaliwakilisha tu kile kilichosemwa jana kwenye kikao cha wanafamilia.

"Sasa hilo si suala la polisi? Si uende polisi kuulizia wamefikia wapi?" alijibu Neema akiwa haelewi mumewe alikuwa na maana gani.

"Nina maana wewe unajua kinachoendelea. Huyu jamaa atakuwa mtu wako ndiyo maana hakuna taarifa yoyote, wala simu yoyote kutoka kwa watekaji."

"Una maana gani baba Diana?"

"Umeshaelewa, mimi sihitaji tena kuwa mfafanuzi."

"Ndiyo hicho kikao chenu cha jana mlichoenda kukaa na ndugu zako? Kumbe mmekwenda kunikalia mimi kuwa mtoto katekwa na mtu ambaye labda ni alikuwa mpenzi wangu, kamchukua mtoto wake kwa nguvu?"

"Siyo hivyo, inawezekana alikuwa anadai mtoto wake, akaona bora amteke."

"Baba Diana una wazimu. Umeshanifanya mimi kahaba ambaye nimepata mtoto mmoja mwenye baba wawili eee.

Sasa nasema hivi. Mimi kwa sasa siondoki hadi nijue hatma ya mtoto. Naomba Mungu mtoto awe hai, arudi kwenye mikono yetu, halafu tukapime DNA, baada ya hapo mimi nitachukua uamuzi unaofaa." Alisema kwa hasira na baada ya hapo, Neema akaangua kilio.

*****************************************

Alikuwa amefika maeneo ya Mtoni kwa Aziz Ally. Bado alikuwa anakanyaga mafuta kuelekea nyumbani kwake akitokea Mbagala kwenye shughuli zake.

Alikuwa anakumbuka mazungumzo yake na Neema siku tatu zilizopita juu ya kupata taarifa kutoka kwenye jumba aliloingia mtekaji kule Ubungo Maziwa.

Kwa sababu hakutaka kuwahusisha polisi, wala mume wa Neema, badala yake ni yeye peke yake na Neema, aliamua afanye kitu kimoja.

Alekee hadi huko. Pale getini kuna mlinzi. Ambacho alitaka kukifanya ni kumsubiri mlinzi yule aliyemkuta siku ile amalize zamu na amfuate na kutengeneza urafiki.

Alijua kabisa akishatengeneza urafiki kwa kumlaghai kwa vipesa kidogo anaweza kupata habari za mtoto yule, tangu alivyoingizwa mle ndani, yupo hai? Anafanya nini? Na kwa sasa bado yupo kwenye jumba lile au amepelekwa wapi.

Baada ya hapo ndipo akakapofanya uamuzi mwingine ambao utakuwa wa manufaa kwa wakati huo.

Wakati akifikiria hivyo kwa mbali, alimuona mwanamke mmoja ambaye ni kama anamfahamu. Alikuwa amesimama kwenye kituoni. Sura yake haikuwa ngeni sana kwa mwanamke huyo, japo alionekana kunenepa tofauti na alivyokuwa awali.

Alipunguza mwendo na kusimamisha gari sehemu salama. Aliteremka na kurudi nyuma. Lengo ilikuwa kumfuata yule mwanamke.

Alikuwa amesimama pale pale. Alionekana kusubiri usafiri wa daladala. Alimfikia karibu "Atakuwa ni yeye." Jerry alijisemea moyoni "Ester." Aliita kwa mashaka.

Mwanamke aligeuka ili kumwona huyo mtu ameyemtaja jina.

Sasa kila mmoja alimwona mwenzake vizuri zaidi. Wakatambuana. Wakakumbaniana kwa furaha.

Yaliyofauta hapo ni mazungumzo ya salaam na kukumbushiana yale ya zamani. Ni watu wanaotambuana.

"Nilidhani nitakuja kukuoa Ester, lakini ukahama chuo sikukuona tena."

"Mpenzi, si unajua tena wazazi, walinihamisha kwa nguvu bila kupenda. Kusema kweli nililia sana. Nikakukumbusha sana mpenzi wangu. Leo ni zaidi miaka kumi ndiyo tunaonana kweli Mungu mkubwa."

"Umeoa Jerry?"

"Bado"

"Unasubiri nini?"

"Sijui hata ninachosubiri, ila bado, wewe je?"

Ester alishusha pumzi, kitu ambacho kilimfanya Jerry kujua kuwa itakuwa ni historia ndefu.

Akamtaarifu kuwa amepaki gari mbele, hivyo atamsogeza anakokwenda.

Walikiwa ndani ya gari, Jerry aliurudia swali.

"Nilikuuliza, mwenzangu, mpenzi wangu wa zamani wakati tuko chuo, umeolewa?"

"Niliolewa, lakini..."

"Umeachika?"

"Si bora ningeachika, ningeolewa na mwingine. Hata wewe mpenzi wangu wa zamani ningekwambia unioe."

"Sasa."

"Mwenzangu nimeolewa tena kwa ndoa ya Kanisani, na nimezaa mtoto mmoja na mume wangu, lakini amenitelekeza."

"Duh, pole sana mpenzi kwa yaliyokutokea."

"Kwa sasa unaishi wapi?"

"Naishi Ubungo wa mjomba wangu, ila wakati niko na mume wangu, tulikuwa tunaishi Kunduchi."

"Yeye huyo mumeo kwa sasa yupo wapi?"

"Anaishi na huyo mwanamke wake, tena wameoana kwa ndoa ya kiserikali kwa sababu haruhusiwi tena kuona kanisani."

"Kwa nini hukuweka pingamizi kwenye ndoa yao?"

"Jerry, yaani mimi hakuniambia chochote, alitoweka tu nyumbani, kumbe alikuwa ameshampangia chumba sehemu, akawa anaishi. Nyumbani kurudi ikawa kwa taabu tabu mwisho, wakaoana bila mimi kujua lolote na baada ya ndoa wakahama na hapo walipokuwa wanakaa. Akawa ndiyo amenitelekeza hivyo na mtoto."

INAENDELEA JUMAPILI



# MZEE ABDUL AAPA KUTOMSAMEHE DIAMOND

BAADA ya mwanamuziki maarufu nchini, Diamond Platnumz, kukiri kwamba Salum Nyange ndiye baba yake mzazi, sasa baba yake aliyemlea, mzee Abdul, ameapa kutomsamehe katika maisha yake yote.

Katika mahojiano yake ya hivi karibuni, Diamond, alisikika akisema kwamba tangu mwaka 2000 alitambua yeye sio mtoto wa Mzee Abdul, baada ya baba yake huyo kuwa mbali naye kimalezi.

Alisema tangu siku hiyo alikuwa karibu na baba yake mzazi Salum Nyange, lakini hakutaka jambo hilo lijulikane kutokana na jinsi alivyokuwa akimuheshimu mzee Abdul.

Hata hivyo, Mzee Abdul amesema yote anamuachia Mungu kwani kinachofanyika sasa ni sawa na kumdhalilisha kwa sababu ya jeuri ya fedha.

"Nimesikia kile ambacho Diamond amezungumza, ninachosema namuachia Mungu najua yote yanatokana na jeuri ya fedha. Kuanzia sasa sitaki msaada wake wa aina yoyote na sitaki akanyage wakati nikifa," amesema Mzee Abdul.



## Mkonwe Cicely Tyson afariki dunia

MWIGIZAJI nguli wa Marekani, Cicely Tyson, amefariki dunia akiwa na miaka 96.

Cicely alijizolea umaarufu kwa zaidi ya miaka 70 ya uigizaji wake akihusika kwenye filamu nyingi ambazo alicheza kama mtu kutoka Afrika ndani ya Marekani. Taarifa iliyotolewa na meneja wake, Larry Thompson, haijaweka wazi chanzo cha kifo chake.

Tyson amewahi kushinda tuzo mbalimbali ikiwamo medali ya Rais wa Marekani 'Presidential Medal of Freedom', mwaka 2016 ambayo alikabidhiwa na Rais wa Marekani wakati huo Barack Obama.

Cicely Tyson alikuwa mwanamke wa kwanza mweusi kupata nafasi ya kuigiza kama mhusika mkuu kwenye igizo la Television 'East Side/West Side' mwaka 1960.



## Tamasha la muziki kufanyika Februari

UBALOZI wa Ufaransa na timu ya ASEDEVA, wametambulisha tamasha jipya la burudani lijulikanalo kwa jina la 'Muziki Wetu Showcase'.

Tamasha hilo litaanza Februari 4, mwaka huu katika ukumbi wa Alliance Francaise, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana , Mkuu wa masuala ya Ushirikiano na Utamaduni, Cecile Frobert, alisema tamasha hilo ni jukwaa jipya la muziki mubashara kwa wasanii kutoka sehemu mbalimbali.

Alisema kusudi la tamasha hilo litawapa fursa wanamitindo kuonyesha sanaa zao, wanamuziki wachanga kuibua vipaji vyao hasa kwa wanawake.

"Litakuwa jukwaa la kuonyesha muziki mubashara litasindikizwa na msanii kutoka Uganda, Sandra Nankoma na Shabo Makato kutoka Tanzania," alisema Cecile.



# Tuchel: Nitamfanya Werner atabasamu

**LONDON,** England

KOCHA mpya wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesema ni jukumu lake kumrejesha kwenye kiwango chake, Timo Werner na kumfanya atabasamu kwa mara nyingine.

Frank Lampard alitimuliwa Jumatatu wiki hii baada ya kuwa na mwenendo mabovu kutokana na kufungwa michezo mitano kati ya minane ya ligi na kuona 'The Blues' wakishuka mpaka nafasi ya 10 na Tuchel kuchaguliwa kuwa mbadala wake.

Kiwango duni cha Chelsea kilisababisha mshambuliaji huyo kuandamwa na ukame wa kufunga na mapaka sasa Werner hajafunga katika michezo 11 ya Ligi Kuu.

"Ni jambo zuri kufanya kazi na nyota wa zamani wa RB Leipzig ambaye hakutumika katika mchezo wa kwanza wa Tuchel tangu achukue mikoba ya kuinoa Chelsea. "Kwa nini sikumtumia Jumatano, niliona uso wake umejifunga kidogo na uzito wake upo mabegani kwake," Tuchel aliwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo wa sare ya bila kufungana na Wolves.

"Anajali sana na hilo linaonyesha kwamba ana tabia njema sana. Muda mwingine kama straika huwa haisadii sana kama unajali sana, muda mwingine unatakiwa kutojali lolote, lakini si mtu wa hivyo anajali sana na hana furaha na yeye mwenyewe na jinsi mambo yanavyokwenda.





# KLOPP, FABINHO WAMUITA MBAPPE

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp na kiungo mkabaji Fabinho, wameripotiwa wote wanamshawishi Kylian Mbappe ajiunge na mabingwa hao wa Ligi Kuu England.

Mustakabali wa Mbappe kwa sasa unazungumziwa sana, na hivi karibuni mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa alikubali kwamba bado hana uhakika ikiwa atasaini mkataba mpya wa muda mrefu na Paris Saint-Germain.

Mkataba uliopo wa mshambuliaji huyo huko Paris unatarajiwa kumalizika Juni 2022, na Liverpool na Real Madrid inasemekana wana hamu kubwa ya kumsajili hivi karibuni.

Kwa mujibu wa Late Football Club, Klopp 'anawashinikiza' wawakilishi wa Mbappe katika jaribio la kumshawishi mshambuliaji huyo aachane na mpango wa mkataba mpya huko PSG ili ajiunge na miamba hao.

Wakati huo huo, kipindi cha Canal + kinadai kwamba Fabinho, ambaye alicheza na kijana huyo pale Monaco, pia amekuwa akiongea na mshindi huyo wa Kombe la Dunia juu ya uwezekano wa kuhamia Anfield.

# Ibrahimovich, Lukaku wapigwa pini Italia

**MILAN,** Italia


BAADA ya kugombana uwanjani katika mchezo wa Coppa Italia, Mshambuliaji wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic na mshambuliaji wa Inter Milan, Romelu Lukaku, wamefungiwa mchezo mmoja.

Ibrahimovic amefungiwa mchezo mmoja baada ya kupatiwa kadi mbili za njano katika mchezo mmoja.

Lukaku amefungiwa kwa sababu kadi ya njano aliyoipata kwenye mchezo huo, ilikuwa ni ya pili kwenye mashindano hayo msimu huu.

Ibrahimovic alikanusha kuwa alitumia maneno ya kibaguzi kwenye tukio lile, licha ya kwamba anafanyiwa uchunguzi katika kile kilichotokea.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii, Ibrahimovic aliweka chapisho lililosomeka "kwenye dunia ya Zlatan, hakuna nafasi ya ubaguzi."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND KUPEWA VIATU VYA AGUERO MAN CITY

●●● Chelsea, Man United na Real Madrid pia zinaaminika kuhitaji saini ya Haaland, lakini...

**MANCHSTER,** England

MANCESTER City imeripotiwa kwamba, imeweka kipaumbele katika kuisaka saini ya mshambuliaji mpya wa kati katika msimu wa usajili wa majira ya joto, Erling Braut Haaland, akipewa nafasi kubwa.

Mkataba wa Sergio Aguero kwenye dimbani Etihad unatarajiwa kumalizika msimu huu wa majira ya joto, na mchezaji huyo wa miaka 32, anaweza kuruhusiwa kuondoka kwa uhamisho wa bure, baada ya kupambana na majeraha msimu huu wa 2020-21 akiwa na Man City.

**Gabriel Jesus amefunga mabao mawili tu ya Ligi Kuu msimu huu, na kocha mkuu Pep Guardiola hivi karibuni amependelea kuwatumia zaidi Kevin De Bruyne na Riyad Mahrez katikati.**

Kwa mujibu wa Manchester Evening News, kipaumbele cha Man City kuelekea kampeni ya 2021-22 ni kusaini mshambuliaji mpya, na Guardiola ameridhika na namba zake kwenye safu ya ulinzi na kiungo.

Licha ya ripoti kutotaja ni nani hasa wanamlenga, hivi karibuni Haaland wa Borussia Dortmund amehusishwa sana na kuhamia kwa miamba hawa wa Manchester.

Mchezaji huyo wa miaka 20, amekuwa akifanya vizuri na Dortmund katika msimu huu, akigusa wavu mara 21 katika mechi 19 klabuni hapo, lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway anaweza kuruhusiwa kuondoka majira ya joto ya 2022.

Chelsea, Manchester United na Real Madrid pia zinaaminika kuhitaji saini ya Haaland.

## ZISIKUPITE

### GUARDIOLA KUMPOTEZEA ALABA

KIKOSI cha Pep Guardiola, hakivutiwi kumsajili beki wa Bayern Munich na Austria, David Alaba, 28, katika dirisha hili la Januari ama majira ya joto, na badala yake klabu hiyo inamulika zaidi kwenye kusajili mshambuliaji. ***(Manchester Evening News)***

### RAMOS, REAL HAKIJAELEWEKA

BEKI wa Hispania, Sergio Ramos, 34, bado hajakubaliana mkataba mpya na Real Madrid, ikiwa ni mwezi mmoja sasa baada ya pande hizo mbili kukutana kujadili kuhusu uwezekano wa kuongeza mkataba wa awali ambao unatarajiwa kumalizika majira haya ya joto. ***(Marca)***

### S'AMPTON NA MAITLAND-NILES

SOUTHAMPTON inajaribu kuipata saini ya beki wa pembeni/kiungo wa Arsenal na England, Ainsley Maitland-Niles, 23, kwa mkopo kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa kesho Jumatatu, lakini pia West Brom nayo ikielezwa kuvutiwa na mchezaji huyo. ***(Sun)***

### MATIP AIPEKA LIVER SOKONI

MIAMBA ya Anfield, Liverpool, ilipanga kutumia saa 72 za mwisho (kuanzia jana) kabla ya dirisha dogo la usajili kufungwa kesho, kutoa ofa ya dakika za mwisho kusajili beki wakati baada ya Joel Matip naye kujiunga katika orodha ya wachezaji waliopo chumba cha majeruhi. ***(Telegraph)***

### MADRID BADO NA MBAPPE

REAL Madrid itafunga safari kwenda kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa na Paris St-Germain, Kylian Mbappe (22), majira haya ya joto. ***(Marca)***

### KUMLETEA POCHETTINO DELE

KLABU ya Paris St-Germain ipo tayari kumuunganisha kocha Mauricio Pochettino na kiungo wa Tottenham, Dele Alli, 24, kutokana na miamba hiyo ya Ligue 1 kuamini kwamba nyota huyo wa England atahitaji kubaki hapo kwa muda mrefu pindi atakapoizoea klabu hiyo. ***(Eurosport)***

### LIVERPOOL KUMFUATA LONG

LIVERPOOL inapanga kwenda kumsajili kwa mkopo beki wa New York Red Bulls na Marekani, Aaron Long, 28. ***(ESPN)***

### ROSE ANUKIA KUTUA UTURUKI

KLABU ya Uturuki, Trabzonspor, inaamini kwamba imefikia makubaliano ya kumsajili beki wa kushoto wa Tottenham na England, Danny Rose, 30. ***(Talksport)***

### GRAY AKARIBIA LEVERKUSEN

LEICESTER City na winga wa England, Demarai Gray, 24, amekubaliana malipo binafsi na miamba ya Bundesliga, Bayer Leverkusen, lakini bado kuna mvutano wa ada ya uhamisho kwa klabu hizo mbili. ***(Bild - in German)***

## HABARI MICHEZO

# TP MAZEMBE YATEGA NDOANO KWA BWALYA

**Na Mwandishi Wetu**

KIWANGO cha kiungo wa Simba, Mzambia Rally Bwalya, kimewavutia mabosi wa mabingwa wa DR Congo, TP Mazembe, hivyo kuingia katika rada za wachezaji wanaohitaji huduma yao, imefahamika.

**Bwalya ambaye alionyesha kiwango cha juu kwenye mechi zote mbili za kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe, ameendelea kuwa msaada mkubwa katika mechi zote alizoichezea timu hiyo kuanzia hapo.**

Katika mechi ya Simba Super Cup dhidi ya Al Hilal ya Sudan, ambayo Simba iliibuka na ushindi wa mabao 4-1, Bwalya pia alionyesha kiwango cha juu huku akifunga bao moja.

Akizungumza na gazeti hili juzi kwa sharti la kutotajwa jina kwa kuwa si msemaji wa klabu hiyo, mjumbe mmoja wa bodi ya Simba aliyeko katika kamati ya maandalizi ya michuano ya Simba Super Cup, alisema TP Mazembe wamevutiwa na Bwalya na wameonyesha nia ya kuipata huduma yake.

"Bwalya amewavutia sana TP Mazembe na wamesema wamekuwa wakimfuatilia katika mechi ambazo ameichezea Simba hivi karibuni, wameulizia uwezekano wa kumpata, wakasema wakirudi kwao wataleta ombi rasmi," alisema mtoa habari wetu.

Hata hivyo, tayari Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, hivi karibuni alisema kwa sasa ni vigumu klabu hiyo kuuza wachezaji wake kutokana na Mwekezaji na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji, kutaka kuijenga klabu hiyo kwanza.

Manara alisema pia kuna klabu moja ya Ulaya ilikuwa tayari kuweka mezani zaidi ya Sh. bilioni moja za Tanzania ili kuipata huduma ya Luis Miquissone, lakini Mo alitia ngumu akisema kama inataka itoe bilioni mbili.

Bwalya anatarajiwa kushuka tena Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam leo kutoa burudani kwa mashabiki wa Simba itakapoivaa TP Mazembe kwenye mechi ya kuhitimisha michuano ya Simba Super Cup maalum kwa ajili ya kujiandaa na hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na Ligi Kuu Bara.

## CAS yamrejesha Ahmad urais CAF

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Usuluhishi wa Michezo ya Kimataifa (CAS), imemrejesha kwa muda madarakani Ahmad Ahmad kama Rais wa Shirikisho la Soka la barani Afrika, CAF.

Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka duniani (FIFA), Novemba 19, mwaka jana ilimfungia Ahmad kujihusisha na soka kwa kipindi cha miaka mitano, baada ya kumkuta na hatia ya kukiuka kanuni kadhaa za maadili za uongozi wa soka.

Kifungo hicho kilikuwa na maana kuwa Ahmad alipoteza haki yake ya kugombea tena katika uchaguzi Mkuu wa CAF utakaofanyika Machi 12, mwaka huu, lakini alikata rufaa CAS na kuomba adhabu yake iondolewe kwanza hadi rufaa yake itakaposikilizwa.

## Biashara yaanza kujiwinda Ligi Kuu

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara ukitarajiwa kuanza rasmi Februari 13, mwaka huu, Biashara United imesema ipo katika maandalizi makali ya kurejea kumpambana.

Timu hiyo inayonolewa na Kocha Mkuu, Francis Baraza, ipo nafasi ya nne kwenye msimamo ikiwa imejikusanyia jumla ya pointi 29 baada ya mechi 18 na inashika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Yanga ilicheza mechi 18, ndiyo iliyopo kileleni ikiwa na alama 44 tisa mbele ya Simba yenye mechi tatu mkononi, huku Azam ikishika nafasi ya tatu kwa pointi zake 32 baada ya kushuka dimbani mara 17.

Ofisa Habari wa Biashara United, Idrisa Sechombo, amemwambia mwandishi wetu kuwa wachezaji wa timu hiyo wamerejea mazoezini baada ya kumaliza mapumziko mafupi waliopewa.




Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, akimvisha mkanda wa ubingwa wa mabara wa uzito wa light, bondia Ibrahim Class, baada ya kumtwanga kwa pointi bondia Dennis Mwale wa Malawi, kwenye pambano lililofanyika Ukumbi wa Next Door Arena, Masaki jijini Dar es Salaam. Wanaoshuhudia tukio hilo ni Mkurugenzi wa Maendeleo wa Michezo nchini, Yusuph Singo (kulia kwake) na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Jackson Group Sports, Kelvin Twissa (kushoto kwake), ambaye aliandaa pambano hilo. **MPIGAPICHA WETU**

# *Class, Jongo watwaa ubingwa wa WBF*

**Mwandishi Wetu**

WATANZANIA Ibrahim Class na Jongo Shaban wamefanya kweli kwenye pambano la The Rumble in Dar kwa kushinda mikanda ya ubingwa wa WBF wa mabara na International.

Ushindi wa mabondia umeongeza furaha ya mashabiki wa ndondi nchini ambao wamesema haukuwa na kona kona huku wakiipongeza Kampuni ya Jackson Group Sports kwa kuandaa pambano hilo kubwa lililoonyeshwa kwenye nchi 150 duniani.

Akicheza nyumbani, Class alionyesha nidhamu ya mchezo na ubora vilivyomsaidia kuongoza raundi zote 12 na kutawazwa bingwa mpya wa mabara wa WBF kwa pointi za majaji wote dhidi ya Dennis Mwale wa Malawi.

Jongo alimchapa kwa TKO raundi ya kwanza Shawn Miller wa Marekani ambaye aliumia mkono wa kushoto na kushindwa kuendelea na pambano hilo lililopigwa kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Masaki jijini Dar es Salaam na kudhamini na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Benki ya CRDB na Hoteli ya Onomo.

Wakizungumzia ushindi wao, mabondia hao walisema hiyo ndiyo ilikuwa ndoto yao huku Class akibainisha kukutana na upinzani mkali kutoka kwa Mwale.

"Nilianza kwa kumsoma raundi ya kwanza, Mwale ni bondia hachoki, harudi nyuma na muda wote ana uchu wa kushambulia, ila uzoefu, mazoezi na maelekezo ya kocha wangu baada ya kuisha raundi ya kwanza vilinisaidia," alisema.

Katika pambano hilo, Mwale alianza kwa nguvu na spidi akionekana kutaka kumaliza mchezo mapema, alirusha ngumi nyingi, lakini si zote zilizomlenga Class ambaye alicheza kwa kujihami na kushambulia kwa kushtukiza katika raundi hiyo.

Class alirudi vizuri na kumshambulia Mwale raundi ya pili hali iliyoamsha furaha kwa mashabiki wake waliomshangilia wakiimba na kulitaja jina la bondia huyo, akionyesha utulivu hadi raundi ya 12 alipotangazwa kuwa bingwa mpya wa WBF wa mabara kwenye uzani wa super feather.

"Ni mara yangu ya kwanza kupigwa, nimecheza na bondia na pambano lilikuwa gumu, nimpongeze tu kwa ushindi," alisema Mwale muda mfupi baada ya pambano hilo.

Jongo bingwa mpya wa WBF International kwenye uzani wa juu, alisema amefarijika kwa kuendelea kupata matokeo yasiyokuwa na utata na kutwaa ubingwa huo.

Mara ya mwisho, Jongo alimchapa kwa KO, Alphonce Mchumiatumbo bondia namba moja nchini kwenye uzani wa juu kabla ya usiku wa kuamkia jana kuendeleza ubabe kwa Miller.

Pambano lingine lililokuwa gumzo ni lile la Tervel Pulev aliyeshinda kwa Technical Knock Out (TKO) dhidi ya Vikapita Merero wa Namibia katika raundi ya tisa ya pambano lililokuwa la raundi 10.

Nasibu Ramadhan alishinda kwa KO dhidi ya Nkosinati Biyana wa Afrika Kusini dakika ya 1:27 ya raundi ya pili, Kaminja Ramadhan aliweka rekodi ya kupigwa kwa KO ya mapema kwenye The Rumble in Dar.

Bondia huyo wa uzani wa Cruiser alichapwa dakika ya pili ya raundi ya kwanza na Hafidh David huku Happy Daudi akipigwa na Mzambia Lolita Ndembo.

Mkurugenzi wa Jackson Group, Kelvin Twissa, alisema huo ni mwanzo wa kueleta mapambano makubwa nchini, mashabiki wa ndondi wajiandae uhondo zaidi kwenye The Rumble in Dar 2, Machi mwaka huu.

"Pambano hili limeonyeshwa katika nchi 150 duniani, hii ni hatua kubwa kwetu kama waandaaji, limefanyika kwa mafanikio na litakalokuja litakuwa ni kubwa zaidi," alisema.

# Michezo

Jumapili Januari 31, 2021

Nipashe




## Haaland kupewa viatu vya Aguero Man City

HABARI UK 22

**KWA UFUPI**

### CAS yamrejesha Ahmad urais CAF

**Na Mwandishi Wetu**



MAHAKAMA ya Usuluhishi wa Michezo ya Kimataifa (CAS), imemrejesha kwa muda madarakani Ahmad Ahmad kama Rais wa Shirikisho la Soka la barani Afrika, CAF.

UK. 23

### Class, Jongo watwaa ubingwa wa WBF

**Mwandishi Wetu**



WATANZANIA Ibrahim Class na Jongo Shaban wamefanya kweli kwenye pambano la The Rumble in Dar kwa kushinda mikanda ya ubingwa wa WBF wa mabara na International.

UK. 23

**ACHIA SHUTI...**



Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, akitoa maelekezo kwa kiungo wa timu hiyo, Clatous Chama, wakati wa mazoezi ya kujiandaa na michuano ya Simba Super Cup. Pembeni ni Mtaribu wa timu hiyo, Abbas Ally. **MPIGAPICHA WETU**.

# SIMBA, TP MAZEMBE NI ZAIDI YA FAINALI LEO

## ●●●Zuchu kunogesha kwa Sukari mechi hiyo ya kihistoria, bingwa kuondoka na mil. 15/-, makocha wote watamba wakieleza....

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

MABINGWA wa soka Tanzania Bara, Simba, leo watakuwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza dhidi ya Mabingwa wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, TP Mazembe, kwenye mechi ya kuhitimisha michuano maalum ya Simba Super Cup iliyoanza Jumatano wiki hii ikishirisha timu tatu, nyingine ikiwa ni Al Hilal ya Sudan.

Ni michuano mifupi iliyoanzishwa kwa lengo ya kuzipa timu hizo maandalizi mazuri ya Ligi ya Mabingwa ngazi ya makundi, ilianza kwa wenyeji Simba kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Al Hilal kabla ya Wasudan hao juzi kuzinduka na kuichapa TP Mazembe 2-1.

Ni michuano iliyozishirikisha timu tatu ambazo zote zipo kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa, Simba ikiwa Kundi A sambamba na AS Vita ya DR Congo na Al Merrikh ya Sudan, wakati TP Mazembe na Al Hilal zenyewe zikiwa kwenye Kundi B pamoja na CR Belouizdad ya Algeria na Melodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Ili Simba iweze kutwaa kombe hilo linalokwenda sambamba na zawadi ya Sh. milioni 15 kwa bingwa wa michuano hiyo, inatakiwa ishinde, itoke sare au isifungwe mabao 4-0.

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes Da Rosa, amesema mechi hiyo itakuwa ngumu, lakini amewaelekeza wachezaji wake jinsi ya kufanya dhidi ya timu hiyo ngumu Afrika.

"Nahitaji kupata ushindi na kuhakikisha kombe linabaki nyumbani, ni mashindano mazuri yamenipa mwanga wa kuwajua wachezaji wangu na kuona jinsi gani walivyoingia katika mfumo katika hizi siku chache za mazoezi," alisema Gomes.

Naye Nahodha wa Simba, Mohammed Hussein 'Tshabalala', alisema wamejipanga vizuri na watawapa burudani mashabiki kuhakikisha wanapambana kucheza soka la kibingwa.

"TP Mazembe si mara ya kwanza kukutana nao, tunaenda kupambana kwa ajili ya mechi yetu hiyo, hatuna hofu nao kabisa," alisema Tshabalala.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa TP Mazembe, Felix Mwamba, alisema wamepoteza mechi dhidi ya Al Hilal na wataingia uwanjani kwa kutafuta ushindi na hawatakuwa tayari kufungwa na Simba.

"Mechi ile hatukuwa na bahati, hatukucheza kwa umakini, Al Hilal walikuwa wanazuia muda mwingi na kushambulia kwa kushtukiza kwa sababu mawinga wao walikuwa na mbio, lakini kwenye mechi ya Simba naamini tutashinda na wachezaji wetu tumeshawaambia hivyo.

"Tutabadilisha kikosi kabisa hatutaanza na kile kilichoanza dhidi ya Al Hilal, kama Simba hawajawahi kufungwa kwao sasa naahidi tutawafunga na kuondoka na kombe," alisema Mwamba.

Hii itakuwa ni mara ya tano kwa Simba kukutana na Wakongomani hao, lakini ikiwa ni mara ya tatu kucheza kwenye Uwanja wa Mkapa. Mechi zote nne ambazo tayari timu hizo zimecheza ilikuwa ni za Ligi ya Mabingwa Afrika, mbili zikiwa ni za hatua za mwanzo, lakini mbili zikiwa ni hatua ya robo fainali.

Machi 2011, TP Mazembe iliitandika Simba mabao 3-1 nchini DR Congo na Aprili kwenye mechi ya marudiano nchini Tanzania Simba ilifungwa mabao 3-2, ikiwa ni raundi ya kwanza ya michuano hiyo, mechi ambayo ilisababisha Wakongo nao kumchukuwa Mbwana Samatta.

Mwaka 2019, timu hizo zilikutana hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa. Katika mechi ya kwanza nchini Tanzania, Simba ililazimishwa suluhu, kabla ya kuchapwa mabao 4-1 nchini DR Congo na kutolewa kwenye hatua hiyo.

Katika hatua nyingine Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, amesema kuwa msanii Zuchu ambaye anafanya vizuri na ngoma yake ya 'Sukari' atatumbuiza kwenye kilele hicho cha Simba Super Cup huku Waziri Habari Utamaduni Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa akitarajiwa kuwa mgeni rasmi .

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042